

**NAFASI YA UTANI WA SOKONI NA DIKONI KWA JAMII YA  
WAZANZIBARI**

**Na**

**Salama Omar Othman**

**Tasnifu kwa Ajili ya Kukamilisha Mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika  
Fasihi ya Kiswahili katika Chuo Kikuu Cha Dodoma**

**Chuo Kikuu cha Dodoma**

**Oktoba, 2015**

## **ITHIBATI**

Aliyetia saini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma hii iitwayo “**Nafasi ya Utani wa Sokoni na Dikoni kwa Jamii ya Wazanzibari**”, na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu cha Dodoma kwa ajili ya kukamilisha masharti ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma

.....

Dkt. Athumani S. Ponera

(Msimamizi)

Tarehe.....

## **IKIRARI NA HAKI MILIKI**

Mimi, Salama Omar Othman, ninathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika chuo kikuu kingine kwa ajili ya shahada yoyote.

Saini.....

Hairuhusiwi kunakili, kutafsiri, kupiga chapa au kuiga sehemu yoyote ya tasnifu hii bila ya ruhusa ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Dodoma.

## **SHUKURANI**

Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijaalia uzima na afya njema, na kuniwezesha kukamilisha masomo yangu kwa vizuri. Pili ninamshukuru msimamizi wa utafiti huu, Dkt Athuman Ponera, ambaye alikuwa muongozaji wa kazi hii, na alihakikisha kazi hii inamalizika ikiwa na ubora unaotakiwa mbali ya kuwa katika kikwazo cha afya yake. Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema ye ye na familia yake.

Aidha, nawashukuru walimu wote walionifundisha kozi za fasihi ya Kiswahili ambao walinisaidia kupanua uelewa wangu hadi kupata mawazo ya kuujengea hoja utafiti huu. Tatu, nawashukuru wazazi wangu, marehemu Bimdogo Hamad na Bwana Omar Othman, kwa kunilea na kunipatia elimu. Mungu awalipe pepo ya juu, amina. Vile vile, ninaishukuru familia yangu yote kwa kunipa moyo juu ya masomo yangu; shukurani zaidi nazitoa kwa mume wangu mpenzi Bwana Saleh Yussuf, kwa kutojali upweke niliomuachia muda wote wa masomo pamoja na ulezi wa watoto wetu. Mwingine dada yangu, Asha Omar, kwa kudhihirisha upendo wake kwangu kunijali katika kipindi kigumu.

Nne, nawashukuru walimu na washauri wangu, Mabwana Bakar Mjaka, Mwalimu Nahoda, na Omar Zeid pamoja na wataalamu wa fasihi kutoka Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) na BAKIZA kwa ushauri na maelekezo yao juu ya kufanikisha utafiti huu. Mwisho niwashukuru wanafunzi wenzangu wa Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili kwa ushirikiano wao. Hapa niwataje wachache: kati yao Mabwana Simba Gora, Amour Said, Ali Haji, pamoja na Mabibi Saida Said na Bimkubwa Hemed kwa kubadilishana mawazo juu ya tafiti zetu. Mungu awaongoze katika kheri.

## **TABARUKU**

Ninaitabaruku tasnifu hii kwa mume wangu mpenzi, Bw Saleh Y. Khatib, na watoto wangu Salma, Suleiman na Salim kwa kunivumilia na kunijali kipindi chote cha masomo yangu. Nawapenda nyote; ipokeeni kazi hii kama zao la upendo unaotushikamanisha.

## **IKISIRI**

Utafiti huu uliangalia nafasi ya utani wa sokoni na dikoni kwa jamii ya Wazanzibari.

Utafiti uliongozwa na malengo matatu ambayo yalisaidia kubainisha nafasi ya utani wa sokoni na dikoni kwa jamii ya Wazanzibari. Tafiti zinazohusu utani nyingi zamezungumzia juu ya utani wa makabila na kwenye matukio ya sherehe na misiba na kutoa nafasi kwa mtafiti kuuchunguza utani katika muktadha huu.

Utafiti ulifanyika uwandani na maktabani, na kutumia mbinu ya usaili, udodosaji, na ushuhudiaji katika kukusanya data. Maeneo yaliyotumika katika ukusanyaji wa data ni soko la Mwanakwerekwe na diko la Maruhubi katika mkoa wa Mjini Magharibi Unguja. Data zilichambuliwa kwa kuongozwa na nadharia ya utambulisho wa kijamii ambayo misingi yake mikuu ni utambulisho wa kijamii, ulinganishi katika jamii pamoja na matabaka na mgawanyiko katika jamii.

Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa utani wa sokoni na dikoni una nafasi kubwa kwa jamii kwa jamii ya Wazanzibari. Utani huzuka kutokana na sababu tofauti za kijamii, kiuchumi na kiutamaduni. Na hujengeka zaidi kwa maneno yenyewe ubeuzi dhihaka na utwezaji; na mara chache hutambwa kimatendo. Aidha, utani umekuwa ni chachu ya kuleta maelewano na udugu kwa watumiaji wa soko na diko na kupeleka mbele gurudumu la maisha yao. Zaidi, utafiti umegundua kuwa jadi hii bado wanajamii wanaikubali na ipo haja ya kuiendeleza kwani utani kwa wao ni kitambulisho cha utamaduni wao. Nadharia ya Utambulisho wa Jamii iliyotumika ilisaidia kufafanua jinsi utani unavyowatambulisha watu kwa hadhi zao, kazi zao na kutofautiana baina yao katika muktadha wa sokoni na dikoni.

## YALIYOMO

ITHIBATI .....	i
IKIRARI NA HAKI MILIKI .....	ii
SHUKURANI .....	iii
TABARUKU .....	.iv
IKISIRI.....	v
YALIYOMO .....	vi
ORODHA YA PICHA .....	.ix
ORODHA YA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA .....	x

<b>SURA YA KWANZA: UTANGULIZI .....</b>	<b>1</b>
1.2 Ufafanuzi wa Istilahi Zilizotumika katika Utafiti .....	1
1.2.1 Kejeli .....	1
1.2.2 Dhihaka .....	2
1.2.3 Diko.....	2
1.2.4 Utani.....	3
1.2.5 Historia ya Utani .....	4
1.2.6 Aina za utani .....	5
1.2.6.1 Utani wa Eneo kwa Eneo .....	6
1.2.6.2 Utani wa Binamu .....	6
1.2.6.3 Utani wa Mashemeji .....	6
1.2.6.4 Utani wa Bibi /Babu na Wajukuu .....	7
1.2.6.5 Utani wa Makundi ya Watu .....	7
1.3 Usuli wa Tatizo la Utafiti .....	8
1.4 Tamko la Utafiti .....	10
1.5 Malengo ya Utafiti .....	11
1.5.1 Lengo la Jumla .....	11
1.5.2 Malengo Mahsus .....	11
1.5.3 Maswali ya Utafiti.....	11
1.6 Manufaa ya Utafiti .....	12
1.7 Nadharia ya Utafiti.....	12
1.8 Hitimisho.....	14

<b>SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDIKO.....</b>	<b>15</b>
2.1 Utangulizi.....	15
2.2 Maandiko YahuSuyo Dhana ya Utani .....	15
2.3 Mapitio kuhusu Utani katika Jamii za Wazanzibari .....	19
2.4 Mapengo ya Utafiti .....	23
2.5 Hitimisho.....	23
<b>SURA YA TATU: USANIFU NA MBINU ZA UTAFITI.....</b>	<b>25</b>
3.1 Utangulizi.....	25
3.2 Mpango waUtafiti .....	25
3.3 Eneo la Utafiti .....	25
3.4 Walengwa wa Utafiti .....	26
3.4.1 Jamii ya Watafitiwa .....	26
3.4.2 Usampulishaji na Sampuli Iliyotumika.....	26
3.5 Ukusanyaji wa Data .....	27
3.5.1 Njia zilizotumika Wakati wa Kukusanya Data .....	27
3.5.1.1 Usaili .....	28
3.5.1.2 Udodosaji .....	28
3.5.1.3 Ushuhudiaji .....	28
3.5.1.4 Udurusu wa Machapisho Maktabani.....	29
3.5.2 Zana Zilizotumika Wakati wa Ukusanyaji wa Data .....	29
3.6 Mchakato wa Ukusanyaji Data na Udhibiti wake.....	29
3.7 Uchambuzi wa Data .....	30
3.8 Mipaka ya Utafiti .....	30
3.9 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi Wake .....	30
3.10 Hitimisho.....	31
<b>SURA YA NNE: UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MATOKEO YA MJADALA WA UTAFITI .....</b>	<b>32</b>
4.1 Utangulizi.....	32
4.2 Taarifa kwa ufupi kuhusu Wazanzibari .....	32
4.2.1 Miktadha ya Maisha ya Wazanzibari.....	32
4.2.1.1 Muktadha wa Kijografia .....	33

4.2.1.2 Muktadha wa Kiuchumi .....	33
4.2.1.3 Muktadha wa Kiutamaduni .....	34
4.2.2 Sababu za Kuzuka kwa Utani wa Sokoni na Dikoni Kwa Jamii ya Wazanzibari .....	35
4.2.2.1 Uhusiano wa Kibiashara kwa Watumiaji na Soko na Diko .....	35
4.2.2.2 Uhusiano wa Kiukoo.....	36
4.2.2.3 Kutambulisha Kazi Anayoifanya .....	37
4.2.2.4 Ugumu wa Kazi Wanazozifanya.....	37
4.3 Muundo wa Utani wa Sokoni na Dikoni.....	38
4.3.1 Sampuli za Matukio ya Utani wa Sokoni na Dikoni.....	39
4.4 Athari za Utani wa Dikoni na Sokoni kwa Jamii ya Wazanzibari .....	51
4.4.1 Tija za Utani.....	51
4.4.1.1 Kuimarisha Umoja na Mshikamano .....	51
4.4.1.2 Kukuza Uvumilivu na Kuzuia Hasira .....	52
4.4.1.3 Kujenga Umaarufu .....	53
4.4.1.4 Hukosoa na kurekebisha jamii .....	54
4.4.1.5 Kuhimiza Ujasiri na Juhudi ya Kufanya kazi .....	54
4.4.2 Madhara ya Utani.....	55
4.4.2.1 Chanzo cha Ugomvi na Uadui .....	55
4.4.2.2 Kuvunjiana Heshima.....	56
4.4.2.3 Kurudisha Nyuma Shughuli za Kimaendeleo .....	57
4.4.2.4 Kuimarisha Utamaduni wa Wazanzibari .....	58
4.4.2.5 Kudunisha Utamaduni wa Mzanzibari.....	59
4.5 Hitimisho.....	60
<b>SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .....</b>	<b>61</b>
5.1 Utangulizi.....	61
5.2 Muhtasari wa Tasnifu.....	61
5.3 Utoshelevu wa Nadharia Iliyotumika .....	62
5.4 Mambo Mapya Yanayoibuliwa na Tasnifu Hii.....	63
5.5 Maoni ya Mtafiti juu ya Utafiti Huu .....	64
5.6 Mapendekezo wa Tafiti Zijazo .....	65
<b>MAREJELEO .....</b>	<b>66</b>
<b>VIAMBATISHO .....</b>	<b>69</b>

## **ORODHA YA PICHA**

Picha namba 1: Mtafiti wa pili kulia akiwafanyia usaili wapishi wa dagaa katika diko la Maruhubi Mjini Zanzibar tarehe 22/12/2014. (utafiti 2015) ).....	71
Picha namba 2: Mtafiti akimuhoji mfanya biashara katika soko la Mwanakwerekwe Zanzibar tarehe 24 /12 /2014 (Utafiti 2015) .....	72
Picha namba 3: Mtafiti akiwa katika mnada wa nazi katika soko la mboga mboga Mombasa Zanzibar tarehe 24/12/2014 (chanzo mtafiti) .....	73
Picha namba 4: Wavuvi wakitaniana utani kimatendo katika diko la maruhubi tarehe 22/12/2014 (Utafiti, 2015) .....	74

## **ORODHA YA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA**

**BAKIZA**

Baraza la Kiswahili Zanzibar

**Bw**

Bwana

**Dkt**

Daktari

**SUZA**

State University of Zanzibar

**TUKI**

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

## **SURA YA KWANZA**

### **UTANGULIZI**

#### **1.1 Utangulizi**

Sura hii inafafanua vipengele vinavyotoa picha kuhusu tasnifu. Nayo ni ufanuzi wa istilahi muhimu, usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, na manufaa ya utafiti.

#### **1.2 Ufanuzi wa Istilahi Zilizotumika katika Utafiti**

##### **1.2.1 Kejeli**

Ntarangwi (2004:106) anaifafanua kejeli au kinaya kuwa ni mbinu katika fasihi ambapo mtunzi hutumia maneno dhidi ya mtu au hali fulani ili kuchekesha au kutania. Kejeli ki kawaida hutoa maana iliyo kinyume na vile ilivyosemwa au kutendwa. Mulokozi na Kahigi (1979) wanaifasili dhana hii ya kejeli kuwa ni usemi amba maana yake ya ndani ni kinyume cha maana ya nje inabeua maana yake halisi. Wataalamu hao wanaichambua zaidi kwa kusema: Kejeli ni usemi wenye kebehi ndani yake ambapo kisemwacho ndicho kibeuliwacho na msemaji. Msokile (1992) anasema kwamba kejeli ni maneno yenyenye dharau, mzaha au kebehi. Naye anatilia mkazo kuwa maana inayopatikana katika kejeli ni kinyume na makusudio halisi. Kwa ujumla kejeli ni kionjo cha fasihi ambacho maneno yake hutoa muono wa kudhihaki kwa kukipa kitu sifa au hadhi isiyokuwa yake.

Mrikaria (2010:107) anasema kwamba kejeli ni maneno au semi ambazo zina kinyume fulani katika usemi, hali au tukio fulani. Kwa mfano mtu fulani amepatwa na janga fulani, marafiki zake huweza kufurahishwa sana moyoni na janga hilo lililompata rafiki yao pale ambapo mtu huyo amekuwa na tabia ya kudharau ushauri wa wenzake.

### **1.2.2 Dhihaka**

Senkoro (1882:13) ameifasili dhana hii ya dhihaka kwa kusema kwamba ni tamathali yenyе ubeuzi mkali itumiayo maneno ambayo yanasi kika vizuri masikioni wakati ambapo yamekusudiwa yatoe maaana iliyo kinyume. Naye Madumulla (2005:146) amefafanua dhana hii kuwa ni maelezo au masimulizi yanayokusudia kubeua jambo na hulenga kudunisha au kudhalilisha.

Tukiangalia chimbuko la neno hili, ambalo ni la Kiarabu lenye maana ya amecheka (*dhabika*), tunaweza kujumuisha fasili hii kwa kusema kwamba dhihaka ni maneno yatolewayo kwa lengo la kudunisha na kubeua ili kumuudhi muhusika na kuifurahisha hadhira. Kwa muktadha wa utafiti huu dhihaka hukaribia kufanana na utani lakini, mtindo unaotumika wa kuuwasilisha dhihaka mara nyingi huwa na vionjo vinavyokwenda kinyume na uhalisi wa mtu anayeambiwa. Mara nyingi kauli za dhihaka hujiegemesha kwenye kusifu kwa sifa isiyokuwepo au kumilikisha kitu kwa asiye na uwezo wa kumiliki kitu fulani. Hivyo, kuonekana wazi kuwa palikuwa na lengo la kudunisha au kudhoofisha hadhi ya muhusika.

### **1.2.3 Diko**

BAKIZA (2010) wanaifasili dhana hii kuwa ni kikwezo cha vyombo vy ya majini hususani vyombo vidogo vidogo kama ngalawa na jahazi. Kwa muktadha wa utafiti huu tunaangalia maana ya diko kuwa ni sehemu ya kushushia samaki ambapo wachuuzi hufika kununua kitoweo na kuuza sehemu tofauti. Kwa upande wa Zanzibar, sehemu hii hutumika kufanya shughuli mbalimbali zinazohusiana na utowezi. Sehemu hii huwa na mkusanyiko wa watu wanaojishughulisha na shughuli tofauti zinazofanikisha upatikanaji wa utowezi kama vile wavuvi, watengenezaji

majahazi, wachuuzi wa samaki, wapishi, wabebaji dagaa na hata wanunuzi wa kawaida ambao wanahitaji utowezi kwa matumizi ya nyumbani.

#### **1.2.4 Utani**

TUKI (2004:446) inafafanua dhana hii ya utani ikitisema ni taratibu za kimila ambazo zinawafanya watu kuambiana au kutendeana jambo lolote bila chuki. Kyando (1993) anaeleza kwamba masihhara ni sehemu ndogo tu ya utani. Na utani ni mahusino yanayojengeka katika jamii yenyе lengo la kukuza ushirikiano na mahusiano baina ya koo, kabilia na familia, ambapo watu huweza kuambiana neno lolote au kuchukuliana vitu bila kuleta athari yoyote. Aidha, Haji (1992) anaueleza utani kwamba ni mpango maalumu unaofuatwa kimila ambao unawafanya watu kuambiana au kutendeana jambo lolote bila chuki. Zaidi, ni kuambiana na kutendeana mambo ya mzaha, dhihaka na bila kuleta taathira yeyote. Naye Sengo na Lucas (1975:14) wanafafanua dhana hii kuwa ni neno la Kiswahili lihusulo mwenendo au utaratibu wa maisha unaoingiliana na mila na desturi kadha wa kadha katika jumuiya za wenyeji wa Afrika Mashariki. Akinukuu kamusi la *American Heritage Mzandi* (2011) uk 32 anasema:

*Jokes are an amusing story with punch, with an affective but incising message. How ever the message and is its presanation is not intended to harm any body. In other word jokes is is a prank or jest. Jokes are usually between peoples with a special relation ship that permit one to tease another without taking offence.*

Utani ni hali ya uchekeshaji ambao ndani yake kuna ujumbe maalum uliokusudiwa kwa mtu kuupata. Hata hivyo, tunaweza kusema ya kuwa utani ni hali ya kufanyiana mzaha, dhihaka masihhara na kutaniana. Kwa kawaida utani hufanywa na watu wenye uhusiano maalumu unaoruhusu watu kutaniana (Tafsiri ya Mtafiti).

Watafiti wameifafanua dhana hii kwa uelewa wao ingawa kwa maneno tofauti lakini yakimaanisha maana ile ile moja. Wako walioifasili dhana hii kwa maana ya mzaha, ucheshi baina ya watu wa kundi fulani kwa mujibu wa makubaliano yao. Wengine walisema ni masihara yanayofanywa na watu wenye uhusiano wakaribu kijamii. Na wengine walisema kwamba ni ujumbe wenye ucheshi amba o huwa umebeba ukweli ndani yake na kuwasilishwa kimzaha. Fasili zote hizo zinalenga lengo moja ambalo ni mzaha wenye kubeba ukweli. Utani ni uhusiano wa kutaniana au kufanyiana masikhara amba o ni tofauti na kutokuheshimiana, na madhumuni yake makubwa ni kupunguza na kuondoa kabisa chuki iliyopo baina ya makundi fulani ya watu. Kwa kawaida utani hufanywa na watu wenye mahusiano ya kiutani japo kidogo na si rahisi kufanya utani kwa mtu usiyemjua. Hata hivyo, utani mara nyengine hutumika ili kumuomba mtu ridhaa ya kuwa mtani wako na asiporidhia basi kanuni haikulazimishi kuendelea kumtania mtu huyo.

### **1.2.5 Historia ya Utani**

Utani ni jambo linalofahamika na watu wengi nchini Tanzania. Utani katika jamii ya Watanzania ni vigumu kupata tarehe ya kuanza kwake. Hata hivyo, vyanzo mbalimbali vinajaribu kunasibisha baadhi ya matukio kuwa ndio chanzo cha utani katika jamii mbalimbali za Tanzania. Sengo katika kufafanua utani wa jamii ya ukwere, anaeleza kwamba chanzo cha utani inasadikiwa kuwa ni vita, njaa na kuwepo kwa biashara ya utumwa. Matukio yote haya yananasibishwa na chimbuko la utani kwa lengo la kujiliwaza kutokana na matatizo yaliyowakabili. Hata hivyo, kwa upande wa sababu ya njaa inasemekana kwamba utani ulikuwa ni kati ya waliopatwa na maafa ya njaa na wale waliokuwa wakiwasaidia. Ama kwa chimbuko la utani katika kisiwa cha Zanzibar, tunaweza kusema ni pale watu walipoanza

kuishi katika kisiwa hicho. Kwani hakuna jamii isiyotekeleza utani katika maisha yao ya kila siku. Hata hivyo, kwa vile hakuna kisa kisicho na sababu basi kuna kauli zinazoelezea asili ya utani kwa jamii ya Wazanzibari. Iddi (2011), akimnukuu Bwana Mrisho Sumbagi wa Tasani Makunduchi, anasema utani haukuwepo Zanzibar tokea awali isipokuwa uliletwa na watu kutoka bara na Wazanzibari waliiga tu. Watu hao ni wale waliofika Zanzibar kwa sababu tofauti kama vile ndowa, biashara, na utamaduni na kuiendeleza amali hii hadi kuonekana ni kitu cha kawaida tu. Hata hivyo, Bwana Makame Mngwali wa Kiuyu anadai kuwa asili ya utani kwa Wazanzibari inatokana na Wazanzibari wenyewe. Dai hili linaweza kupewa nafasi ya karibu kwani, utafiti unaonesha kuwa Wazanzibari ni watani na ndio maana hakuna sehemu hata moja ambayo wanakusanyika kwa shughuli yoyote ile bila kutaniana. Pamoja na utani kutendeka katika kila nyanja ya maisha ya Wazanzibari, bado jamii ya Wakojani iliyoko katika kisiwa cha Pemba inasifika zaidi kwa kutekeleza kwa vitendo jadi hii ya utani na kuufanya utani kama ni sehemu ya maisha yao. Watani wao wakubwa ni wale wa Kiuyu Minungwini.

Kwa mantiki hiyo, utani kwa jamii ya Wazanzibari umeibuka kwa wazaliwa hasa Wazanzibar wenyewe na papo hapo, mwingiliano wa watu umeliimarisha suala la utani kwa Wazanzibari.

### **1.2.6 Aina za utani**

Wataalamu wengi wameugawa utani katika sehemu nne. Utani wa makabila, utani wa binamu, utani wa mjomba na mpwawe, na utani wa bibi au babu na wajukuu zao. Ama kwa upande wa Wazanzibari, tunaweza kuuangalia utani kwa aina tano zifuatazo:

### **1.2.6.1 Utani wa Eneo kwa Eneo**

Huu unajumuisha mji na mji. Katika aina hii watani hutanihana kwa kubeuana na maeneo wanakotoka. Watu hao hutanihana kiasi cha kuweza kuanza salamu kwa matusi kama kielelezo cha utani. Kwa mfano, watu wa Kiuyu watani wao ni Wakojani watu wa Wingwi watani wao ni watu wa Maziwan'gombe.

### **1.2.6.2 Utani wa Binamu**

Huu ni utani unaohusisha watoto waliozaliwa na mjomba au shangazi na watoto waliozaliwa na mama mdogo au mama mkubwa. Mboga (1975) amezungumzia mahusiano ya utani wa kibinamu kuwa, kwa mila za Wayao watani hawa wanaruhusiwa kuoana. Jambo hili linakubaliwa na takribani na makabila yote Tanzania ikiwemo Zanzibar. Watoto hawa wote hawana kipingamizi cha kufunga ndoa na kwa Zanzibar hapo kale ilikuwa ndio jambo la kawida mabinamu kuoana ilifanywa kwa makusudi ya kuhifadhi urithi wa koo husika usiende mbali. Uhusiano wa kiutani kwa watu hawa huwa wa maneno na matendo. Kwa mfano mtoto wa kiume wa mjomba anapofunga ndoa nje ya ukoo wao anaweza kuambiwa ameowa mke mbaya hata kama ni mzuri.

### **1.2.6.3 Utani wa Mashemeji**

Huu ni utani kati ya mke na ndugu wa mume au mume na ndugu wa mke. Katika aina hii mashemeji hutanihana, hadi kufikia mtu kuweza kumwita mke wa kaka yake kuwa mkewe na kumuamuru kumuandalia chakula, au maji ya kukoga kama anavyofanya kwa kaka yake. Katika utani wa mashemeji tahadhari inatolewa kuwa utani huu ufanywe kwa kuzingatia mipaka kwani unaweza kuzua ugomvi pale mmoja wapo atakapovuka mipaka na kusababisha mifarakanano katika familia.

#### **1.2.6.4 Utani wa Bibi /Babu na Wajukuu**

Huu ni utani uanaofanywa kwa kutoa nafasi kwa bibi kuwa karibu na wajukuu zake. Katika aina hii ya utani babu huthubutu kumwita mjukuu wake wa kike mke, na bibi huweza kumwita mjukuu wake wa kiume mume. Ogacho (1974) na Chogero (1975) wamezungumzia mahusiano ya utani baina ya babu, bibi na wajukuu zake na kusema kuwa; wajukuu wanaweza huwa huru kuuliza maswali na kujifunza mambo mbalimbali ya kimaisha ikiwemo uwajibikaji katika kazi, dawa za asili, utunzaji wa familia na masuala ya ndoa. Uhusiano wao wa kiutani huwa endelevu hata baada ya bibi au babu kufariki. Wakati wa msiba wa marehemu wajukuu wanaweza kufanya utani kwa wazee wao, na hawatulii mpaka wazee watoe pesa ndio salama ipatikane. Kwa mfano wajukuu wanaweza kudai mchele wafanye bumbwi wakishapewa basi watatwanga na kutengeneza huku wakimuigiza bibi au babu yao yale aliyokuwa akiyafanya wakati wa uhai wake.

#### **1.2.6.5 Utani wa Makundi ya Watu**

Hii ni aina ya utani inayopatikana katika mzunguko wa shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii, kama vile maofisini, sokoni, bandarini, mashuleni na dikoni. Katika utani huu utani hufanyika kwa namna tofauti na zile za mwanzo ambapo mchanganyiko wa damu kiukoo unakuwepo. Muktadha huu huzingatia zaidi mahusiano ya kikazi, hivyo malumbano ya kiutani huzunguka sehemu hizo. Katika sehemu hizo watu wanaweza kupeana majina ya kiutani tofauti tofauti; na kujenga muamala mzuri kati yao kiasi cha kufikia kupeana mambo ya ndani ya familia zao. Katika sehemu hizi, utani hushamiri zaidi kulinga na matukio yanayojiri kila siku katika jamii. Kwa mfano, kama jana mmoja wa watani wa kundi fulani aliowa basi utani utazunguka duara hili la ndoa. Pamoja na hayo, ikiwa jana kulikuwa na

pambano la mpira kati ya timu fulani asubuhi yake makundi ya watani yatazungumzia jambo hilo.

### **1.3 Usuli wa Tatizo la Utafiti**

Utani sio neno geni katika masikio ya wasomaji na wasikilizaji katika jamii ya Tanzania, Afrika na dunia yote kwa ujumla. Nje ya bara la Afrika, utani huchukuliwa kuwa ni mzaha au ucheshi tu. Katika Bara la Afrika hususani Tanzania, utani pamoja na kuwa na lengo la kuburudisha au kuchekesha, lakini pia una maana zaidi ya mzaha kama unavyochukuliwa na watu wengine duniani. Hapa Tanzania utani ni kielelezo kimoja wapo kinachotambulisha mila na desturi za jamii mbalimbali zinazoizunguka Tanzania.

Utani ni moja kati ya tanzu zafasihi simulizi. Utani kama fasihi simulizi hutofautiana na mabishano yafanywayo juu ya jambo fulani, na ndio maana katika utani tunapata wahusika (watani), tukio kama vile harusi, misiba, mikusanyiko ya biashara, na mwisho ni muktadha ambapo utani unatokea. Utani huweza kuwa muongozo wa wanajamii katika matukio mbalimbali ya kila siku na kuonesha dhahiri kuwa binadamu ni kiumbe anayetofautiana na viumbe wengine kama vile wanyama na miti. Bwana Akida, katika Sengo na Lucas (1975), anasisitiza kuwa ni muhimu kuiendeleza jadi hii ya utani sisi wenyewe kwani “mvunja nchi ni mwananchi”. Hivyo, thamani ya kuuhuisha utani inajulikana zaidi na watendaji utani.

Utani unaweza kuwa chanzo cha maadili mema maishani. Mtu huweza kuhisi kwamba utani ni jambo la kipuuzi na hauhitajiki katika jamii. Hata hivyo katika hali halisi utani ni nguzo muhimu katika jamii kwani huwaunganisha wanajamii na kujiona kama ndugu wa tumbo moja. Wanajamii hutumia maneno makali yenye

mafumbo na kejeli na wakati mwengine kutumia nyimbo katika kukuza na kudumisha utani. Pia kuondosha tofauti zilizopo baina yao kisiasa, kiutamaduni na kijamii. Zaidi, huweza kuutumia katika kuelezana, kukosoana, kuelekezana kwa kupitia matendo ya utani. Pia utani hujenga mapenzi na maelewano na kuwafanya wanajamii kuweza kuondoleana chuki baina yao kwa kuambizana hadharani yale ambayo mmoja wao yanamuudhi kupitia utani. Ama kwa upande wa Wazanzibari, utani hufanyika katika shughuli za kila siku kama vile sokoni na dikoni, ambapo muingiliano wa watu huwa ni mkubwa. Tokea jua lichomozapo watu huanza pirika zao za kujitafutia riziki hadi matulio ya jua kiasi cha kuutumia utani kama kipozeo cha machofu waliyosulubiana nayo.

Utafiti unaohusu utani umechipuka hapa Tanzania kuanzia miaka ya 1970. Kwa mujibu wa Sengo na Lucas (1975), watafiti wa awali kuumakinikia utani walikuwa ni kikundi cha wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambao waliteuliwa kwenda sehemu za kwao kuchunguza namna utani ulivyo na umuhimu katika makabila yao. Tafiti nyingi zilizofanywa kuhusu utani zimejikita kuangalia zaidi nafasi ya utani kwa ujumla wake kwa kuegemea makabila mbalimbali na baadhi wamejikita katika matukio yanayojitokeza kwa awamu katika jamii kama vile utani wa msibani na harusini matukio ambayo hayatokei kila siku kwa jamii husika. Miongoni mwa watu waliojitokeza kuangalia utani ni kama vile Mgakanzila (2010) aliyetafiti juu ya utani katika kabilia la Wasukuma, naye Ritti (1970) alifanya utafiti juu ya “Mahusiano ya Utani kati ya Waarusha na Wameru”. Mfikiriwa (1971) alifanya utafiti juu ya “Mahusiano ya Utani kwa Kabilia la Wadoe”, Makame (1973) alifanya utafiti juu ya mahusiano ya kiutani ya Wabondei, Sengo na Lucas (1975) wao walitafiti juu ya “Utani na Jamii ya Ukwere”, Benne (1974) alifanya utafiti juu

ya “Utani wa Wamasai” na Mzandi (2011) alitafiti juu ya “Nafasi ya Utani wa Msibani na Harusini kwa Kabilia la Wadigo”. Tafiti hizo ni faafu lakini ipo haja ya kuchunguza athari zake kwani tafiti nyingi zimeonekana kuegemea jamii za upande wa Tanzania Bara. Pia zimeongelea zaidi utani kwa kuhusisha makabila na matukio yanayotokea kwa awamu katika maisha ya kila siku. Kwa vile jamii ya Wazanzibari imezungukwa na bahari na watu wengi hujishughulisha na uvuvi pamoja na kilimo, ni dhahiri kwamba sokoni na dikoni itakuwa ni sehemu yenyе muingiliano wa watu wa jamii tofauti na jinsia tofauti. Utani hutawala zaidi katika wakati wote wa shughuli zinazofanyika hapо kila siku, lakini hakuna maandiko yoyote yaliyoandikwa kuangalia utani katika mandhari ya sokoni na dikoni; kiasi ambacho jamii huona utani ule kuwa ni makelele tu. Hivyo, mtafiti ameona ni vyema kuangalia “Nafasi ya Utani wa Sokoni na Dikoni kwa Jamii ya Wazanzibari” katika mkoa wa Mjini Magharibi, ili kuwapa muelekeo juu ya kuuhuisha au kuuacha.

#### **1.4 Tamko la Utafiti**

Jamii ya Wazanzibari katika maisha yao ya kila siku imekuwa ikitekeleza kwa vitendo utani kupitia shughuli zao za sherehe za arusi, msiba, vilabu vy'a mipira, karata, sokoni na kwenye mikusanyiko mbalimbali. Hata hivyo, watafiti wengi wameuzungumza utani kwa kuelekea zaidi juu ya makabila, na eneo kubwa ambalo watafiti wameliangalia ni sehemu ya Tanzania bara kama walivyoelezwa hapо nyuma, ni watafiti wachache tu ndio walioungalia utani kwa upande wa Tanzania visiwani. Zeid (2011) alitafiti juu ya “Athari za Lugha ya Utani kwa Jamii ya Wapemba”. Naye Iddi (2005) alifanya “Utani Katika Jamii ya Wazanzibari” na kuangalia zaidi utani katika harusi na matanga. Naye Mkubwa (2012) alitafiti juu ya “Dhima za Utani Katika Mazishi ya Matanga ya Wapemba”. Kwa kuhofia kupotea

kwa jadi hii kwa jamii ya Wazanzibari na kuondoa dhana ya kwamba utani unajitokeza katika makabila na matukio ya sherehe na misiba pekee, mtafiti ameelekeza mtazamo wake katika kuangalia nafasi ya utani wa sokoni na dikoni kwa kuiamsha jamii juu ya kudumisha amali hii.

### **1.5 Malengo ya Utafiti**

#### **1.5.1 Lengo la Jumla**

Utafiti huu ulilenga kuchunguza nafasi ya utani wa dikoni na sokoni kwa jamii ya Wazanzibari.

#### **1.5.2 Malengo Mahsus**

- a) Kubainisha sababu za kuzuka utani wa sokoni na dikoni katika jamii ya Wazanzibari zikihusishwa na maisha ya kila siku;
- b) Kuchunguza muundo wa utani wa sokoni na dikoni katika jamii ya Wazanzibari, na;
- c) Kutathmini athari za utendaji wa utani jinsi zinavyohusiana na utamaduni wa Wazanzibari.

#### **1.5.3 Maswali ya Utafiti**

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

- a) Ni sababu zipi zinazochangia kuzuka utani wa sokoni na dikoni katika jamii ya Wazanzibari zikihusishwa na maisha ya kila siku?
- b) Utani wa sokoni na dikoni katika jamii ya Wazanzibari huundwaje? Na;
- c) Ni kwa kiasi gani athari za utendaji wa utani zinahusiana na utamaduni wa Wazanzibari?

## **1.6 Manufaa ya Utafiti**

Tasnifu hii ilitazamiwa kuwa kivutio kwa kunawirisha Fasihi ya Kiswahili kwa kuleta manufaa yafuatayo: Awali ya yote kuongeza maarifa kuhusu taaluma ya fasihi simulizi kuhusiana na utani. Pili, kuisaidia jamii ya Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla kulinda na kuuhifadhi utamaduni wao. Tatu kuisaidia jamii ya Wazanzibari kuelewa umuhimu wa utani katika kuendeleza shughuli zao za kila siku na uhusiano mzuri kati yao. Na hatimae kufikia ukomo kwa utafiti huu kutakua ni chachu kwa mtafiti kutunukiwa Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili.

## **1.7 Nadharia ya Utafiti**

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Utambulisho wa Kijamii. Hivyo ukusanyaji wa data uchambuzi na uwasilishaji wa data hizo uliongozwa na nadharia hiyo ilioasisiwa na Tajfel na Turner (1979). Nadharia hii inaeleza jinsi wanaadamu walivyojijengea silika ya kupenda kujitambulisha na kundi au jamii inayohusiana nayo, kulingana na jinsi walivyo sehemu ya kundi au jamii na kujiwekea mipaka na makundi mengine kwa kujitambulisha kama wamoja. Wananaadharia hawa walipendekeza kuwa nadharia hii kutumika kwa sababu ina misingi mikuu mitatu inayobainisha makundi ya watu yanayoshabihiana na yasiyoshabihiana. Kuwepo kwa makundi haya kunategemea hali na mazingira maalum yanayohusiana na kukubalika na kundi jengine la watu. Nadharia hii imebainisha misingi mikuu mitatu ambayo inaweza kutumika kuongoza utafiti. Misingi hiyo ni;

### **a) Utambulisho wa kijamii**

Hapa, mwanajamii anatambulika kwa wepesi yuko katika kundi gani la jamii kwa kigezo cha mila na desturi zilizopo ambazo amepata kutoka watu anaoishi nao.

**b) Ulinganishi katika jamii**

Mtu mwenyewe anatambua anachoiga kutokana na kuvutiwa na mtu au kundi la watu. Uigaji huo unanasibishwa na kundi la watu analoishi nalo na kuwa moja ya wanajamii kwa kufuata mila na desturi zilizopo.

**c) Matabaka na mgawanyiko wa kijamii**

Hihi ni njia inayoamua mtu yuko kundi gani ambapo anaweza kushiriki jambo lolote bila ya mzozo.

Nadharia hii inazungumzia utambulisho wa jamii na utambulisho wa watu. Ni dhahiri kuwa; utani wa sokoni na dikoni hutambulisha hadhi na mahusiano ya mtu na mtu au kundi na kundi. Kwa mfano dalali huonesha hadhi kwa kutumia kejeli yenye utani pale anapomuuzia mshitiri wake. Mtafiti anaamini nadharia hii kuwa ilitoa msaada mkubwa kubainisha ni kwa namna gani jamii ya Ki-Zanzibari itaweza kuziunganisha jamii zenye mila, itikadi na desturi tofauti. Kwa hiyo, nadharia hii ilisaidia kubainisha jamii ya Wazanzibari kwa msingi wa kwamba utani ni kigezo mojawapo kinachowatambulisha watu katika makundi na maeneo mbalimbali wanayoishi. Kama utani upo katika jamii ya Wazanzibari utani huu unawatambulisha kulingana na kundi walilomo, hadhi walizonazo na shughuli tofauti wazifanyazo kutokana na uwezo na hali zao kiuchumi kijamii na kiutamaduni. Hali hii hutupa taswira kuwa utani hujitokeza kutegemeana na hadhi na makundi fulani ya watu na shauku ya mtu mwenyewe juu ya kupenda kutania au kutaniwa na mtu husika. Kwa hiyo, tunaona kuwa nadharia hii itakuwa faafu kwa utafiti huu.

## **1.8 Hitimisho**

Katika sura hii utafiti umeangalia na kutoa ufanuzi wa istilahi muhimu zinazobeba maudhui ya utafiti huu. Miogoni mwa istilahi hizo ni kejeli, dhihaka, diko, utani. Pia umeeleza usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, na manufaa ya utafiti. Aidha, sura hii ilifafanua nadharia iliyotumika katika utafiti huu ambayo ni Nadharia ya Utambulisho wa Jamii na misingi yake mikuu ni utambulisho katika jamii, ulinganishi katika jamii, na matabaka katika jamii.

## **SURA YA PILI**

### **MAPITIO YA MAANDIKO**

#### **2.1 Utangulizi**

Sura hii inafafanua maandishi mbalimbali yatayohusiana kwa namna moja au nyingine na utafiti huu. Hivyo, kipengele hiki kiliangalia maandiko yanayohusu dhana ya utani kwa ujumla na maandiko yanayohusu jamii ya Zanzibar.

#### **2.2 Maandiko Yahusuyo Dhana ya Utani**

Utani ni amali ambayo hurithiwa kutoka kizazi hadi kizazi hii ina maana kwamba kuwapo kwa utani kati ya makabila na jamii kwa ujumla kunazingatia urithi waliouacha mababu zao.

Mzandi (2011) alifanya utafiti juu ya “Nafasi ya Utani wa Harusini na Msibani kwa Jamii ya Wadigo”. Katika utafiti wake huo alieleza kwamba utani unategemea zaidi juu ya matukio na matendo yanayotendwa na wanajamii. Alijenga hoja ya kwamba uhalali na uthabiti wa utani unapatikana pale utani unapotendeka. Hivyo, alieleza kwamba utani wa harusini na msibani unafanyika wakati wa msiba na wakati wa harusi kwa Wadigo. Na kwamba, unahuisha zaidi ngazi za kifamilia kama bibi kwa mjukuu, mtu na binamu yake na kadhalika. Katika kazi hii mtafiti amegusia zaidi matukio yanayotokea kwa awamu na kutokugusia utani unaotokea kila siku kwenye shughuli za kawaida kama vile sokoni na dikoni. Hivyo, utafiti huu unaziba mwanya ulioachwa na mtafiti huyu. Mgakanzila (2010) amefafanua suala la utendekaji utani wa Wasukuma. Ameugawa utani huo katika vipengele vitano, vinavyojumuisha usimulizi, nyimbo, matendo, furaha na hadithi ndefu. Amefafanua kwamba utani una nafasi kubwa katika kufichua maovu ya jamii furaha na viburudisho. Katika matukio ya kufurahisha ikiwa kama njia ya kuambizana ukweli kupitia maelezo ya utani,

masimulizi pia hubeba dhima ya ukweli na uhalisia. Kwa upande wa utani wa maelezo mafupi mwandishi amefahamisha kwamba utani huu ni ule unaofanywa na mtu mmoja au wawili kulitania kundi la watu kwa lengo la kufurahishana. Amezungumzia pia utani wa masimulizi ambao kwa Wasukuma umejengwa kwa ajili ya kufurahisha na kuburudisha. Utani huu huonekana kufanyika kwa mahojiano yaliyo na lengo la kufichua tabia za watu ambazo huwafanya wacheke na kuburudika. Aidha, aina nyingine ya utani kwa Wasukuma ni utani wa matendo ambao umefafanuliwa kwamba huu hufanyika zaidi wakati wa sherehe za arusi. Wale wanaotaniana hufika katika sughuli hiyo wakafanya utani mpaka wapewe pesa na wasipopewa basi huweza kuharibu shughuli kwa fujo watakazozifanya. Utani huu ni maarufu na unaheshimiwa sana. Utani wa kufurahisha pia ni moja kati ya aina za utani wa Kisukuma ambao hufanywa na watu kwa kuwaiga watu wanavyoangalia wanavyotenda na wanavyofanya vitu fulani katika hali ya kawaida utani huu huwa unapingana na ukweli na hufanywa kwa lengo la kujifurahisha. Pia, utani katika nyimbo za Wasukuma huimbwa kwa kutania na kutoa ujumbe muhimu. Nyimbo hizi za utani huimbwa mbele ya hadhira kupitia majigambo ili kufanya watu wacheke zikiwa na ujumbe maalum. Katika kazi hii mwandishi amezungumzia utani kwa kuuhusisha na jamii ya Wasukuma; na hivyo, kutoa pengo kwa mtafiti kushughulikia utani kwa kuangalia mkusanyiko wa watu mbali mbali wanaotumia soko na diko katika jamii ya Wazanzibari.

Ponera (2010) katika utafiti wake juu ya “Athari za Ufutuhi katika Nathari za Shaaban Robert: Maana, Matumizi na Athari Zake kwa Msomaji” ameugusia utani ingawa kwa uchache kuwa kikawaida hulenga kufurahisha na kuchekesha, na kubainisha maumbo ambayo hujitokeza kuwa ni nyimbo, matendo na kauli fupifupi.

Hata hivyo, anasisitiza kuwa utani mara nyingi hujikita katika miktadha mbali mbali ya maisha yanoyowazunguka watani hao. Hivyo mtarufi aliona ni vyema kuizamia miktadha ya maisha ya wazanzibar kwa kuangalia utani sokoni na dikoni.

Bukanya na wenzake (2005) katika kitabu chao cha *Oral Literature* wanausimulia utani kwa ujumla wake na kufafanua kwamba utani unaosababisha migogoro na migongano unaweza kuonekana kama chanzo cha masimulizi. Utani unategemea zaidi unyonyaji wa migongano katika hali ambayo mara nyingi huleteleza furaha lakini, utani hutokea katika hali mbali mbali kama vile maneno yenyе sauti sawa lakini yanye maana tofauti, hadithi za kuchekesha, kejeli nakadhalika

Davies (2005) anauchambua utani katika nyanja mbili kuu. Kwanza ni utani unaomzingatia mtu mmoja mmoja anapoutumia utani ndani ya kundi dogo la watu naye akiwa mionganini mwao, na kwa kiasi gani utani huo unaathiri mahusiano yao ndani ya kundi na kukosekana kwake. Pili tunawenza kufanya stadi lingalishi kuhusiana na utani kwa ujumla na uhusiano wake na jamii na katika taasisi ambapo utani huo unatendwa. Inawezekena kabisa kuhusisha uhusiano wa utani katika nyanja mbili hizi za kiuchambuzi, lakini tu kwa uangalifu na tahadhari. Kwa vile mtaalamu huyu ameelekeza kwamba utani huonekana katika makundi hivyo mtarufi ameona ni vyema kutarufi na kuthibitisha uwepo wa mahusiano ya kuitani sokoni na dikoni.

Gora (1999) katika *Utenzi wa Suleiman bin Daudi* alionyesha kuwa utani ulikuwepo tangu zama za kale za Mitume. Ulisaidia kuhofisha hasa pale palipozuka vita. Hii inadhihirisha wazi kuwa utani haupo kwa ajili ya kuchekesha, kukejeli, na kufanyiana mzaha tu, bali pia hutumika kumhofisha mpinzani kwa njia ya dharau

hasa katika vita. Kwa mfano, katika beti za 143 hadi 146 Jaluti anamdharaau Suleiman bin Daud kwa maneno haya:

143. Baada ya kumsimamiya  
Jaluti kauliziya  
Ulilolifuatiya  
Nena kijana swaghiri
144. Kama ujile kuwana  
Nakuona bado mwana  
Utakalo rudi tena  
Usiingize hatari
145. Nenda utokeyako  
Miye si mwana mwenzako  
Uliza vyangu vituko  
Kama unayo habari
146. Kidudana kama wewe  
Sifurahi nikuuwe  
Kimbiya ujiokowe  
Huwezi zangu kikiri

Kulingana na maoni ya mtunzi, maneno “kijana” na “kidudana” katika beti hizi yametumika kiutani kuonyesha dharaau. Kazi hii imeonesha kwamba utani ni wa tangu enzi; hivyo, si kitu cha kuzuka kama wengine wanavyoona. Kwa kuzingatia haya, mtafiti ameona ni vyema kuchunguza nafasi ya utani kwa jamii ya Wazanzibari inayoshughulika na watumiaji wa soko na dikoni.

Mfikiriwa (1971) alifanya utafiti juu ya “Uhusiano wa Kiutani katika jamii ya Wadoe”. Alionesa asili ya utani wao watokana na kuchukua kitu kwa nguvu. Hata hivyo, kwao koo ndizo huhesabiwa kama kabilia. Katika utafiti huu, mtafiti ameonesha kwamba utani wa Wadoe umeegeemea zaidi katika utendekaji wa matendo zaidi kuliko maelezo ila hakuonesha nafasi ya utani kwa sehemu zenye mjumuiko wa watu wengi kama sokoni na dikoni kwa jamii hizo.

Sengo na Lucas (1975) walifanya utafiti juu ya “Utani wa Jamii ya Ukwere”. Katika kazi hiyo, wanaeleza kuwa chanzo cha utani katika jamii ya Wakwere ni shida au

matatizo kama vile njaa, vita, na matokeo makubwa yejote. Wameugawa utani katika daraja za kifamilia, kijirani, kibinadamu na kikabila. Wataalamu hawa wanaeleza kwamba lugha inayotumiwa na watani katika jamii si ya kawaida na inakubalika kulingana na muktadha. Hivyo hutumika ili kufurahisha na hapo hapo yakiwa na maana kubwa ndani yake yenye kumjenga na kumtafakarisha mtu anayesikiliza.

Yahaya na wenzake (haina tarehe) katika kazi yao The Structure and Function of Jokes In Tanzania walitafiti juu ya mahusiano ya kiutani kwa kuangalia makabila mbali mbali yanayoizunguka Tanzania. Kazi hii ilieleza pia dhima ya utani katika makabila mbalimbali kuwa ni kuburudisha na kuchekesha. Kwa uwazi katika kazi hii mtani anakuwa kama ni chombo cha kuondoa maovu yaliyopo katika jamii kama vile kunapotokea kifo, mtani huwa ana nguvu na ulazima kushiriki kama ndugu ambapo husaidia kuelezea idadi ya watu wanaohusika kuomba ruhusa kutoka kwa muajiri kwa ajili ya kwenda mazikoni. Mtani mazikoni hutozwa pesa kwa kutegemeana na yejote yule mwenye jukumu la kutoa taarifa ya kifo kisichotarajiwa isipokuwa kwa Wachaga na Wamba watani wana kazi mahsus kama vile kuchimba makaburi na kuwa washereheshaji. Kazi hii ilisaidia kuzua fikra mpya kwa mtafiti kuungalia utendaji wa utani katika mjumuiko wa watu mbalimbali.

### **2.3 Mapitio kuhusu Utani katika Jamii za Wazanzibari**

Mtazamo kuhusu asili ya Wazanzibar hufafanuliwa kwa mitazamo miwili, wapo wanaodai kuwa wazanzibari ni mchanganyiko wa watu wenye makabila tofauti kutoka bara kama vile Bagamoyo, Tanga, Kunduchi na kwengineko. Mtazamo huu unaamini kuwa wazanzibari walifika upwa wa bahari kutohana na shughuli za uvuvi, jambo hili husisitizwa kutohana na shughuli wazifanyazo Wazanzibari. Na ndio

maana hata utafiti huu unajikita katika shughuli zile zile wazifanyazo Wazanzibari yaani uvuvi, udalali na uchuuzi wa samaki huku utani wa sehemu hizo ukichunguzwa.

Mtazamo wa pili ni ule unaodai kuwa wazanzibari ni mchanganyiko wa watu watokao bara Arabu yaani Wapashia, waliokuja kwa kusaidiwa kwa pepo za msimu katika shughuli za kibiashara. Juma (2008) anasisitiza kwa kusema, tunapozungumzia historia ya Zanzibar, hatuna budi kutilia maanani hali ya mchanganyiko wa watu wenye asili ya mataifa mbalimbali kama vile bara Hindi, uarabuni na Uajemi.

Mitazamo hiyo miwili inathibitika kutokana na tamaduni walizonazo Wazanzibari, tamaduni ambazo zinamchanganyiko na kufanana na tamaduni za jamii nyengine ila kinacho tofautiana ni jiogirafia ya pahala na mazingira katika tamaduni nyengine au utani ufanyao sehemu nyengine.ya utamaduni huo. Na ndio maana mtafiti akaangalia utani unaofanyika dikoni na sokoni ili kubaini utafauti unaojitokeza kwenye utani wa sehemu nyengine.

Naye Zeid (2011) alifanya utafiti unaohusu “Athari ya Luga ya Utani kwa Jamii ya Wapemba”. Katika utafiti huo mtafiti ameeleza kuwa katika kisiwa cha Pemba bado utani una nafasi muhimu katika maisha ya kila siku. Kwa vile utani umetawala katika sehemu za jamii, haifikiriwi kama kuna mtu kwa njia moja au nyengine asiyeshiriki katika harakati za utani katika jamii ya Wapemba, na kufahamisha kuwa utani hufanywa katika miktadha ya mazishini, matangani, harusini na katika shughuli za kiuchumi. Pia, mtafiti anaeleza kwamba utani umetawaliwa na semi zenye kuashiria kejeli, dhihaka, matusi, na dharau. Semi hizo hujitokeza na kupotea

na hakuna semi inayotumika daima. Mtafiti amezungumzia utani kwa jamii ya Wapemba lakini aliegemea katika fani ya isimu na alitazama zaidi athari ya vitendo neni katika lugha ya utani. Kutokana na hayo, mtafiti ameona ni vyema kuuangalia utani katika uga wa fasihi hasa katika kisiwa cha Unguja.

Kwa kusisitiza utumiaji wa jadi hii ya utani kwa Wazanzibari, na hasa kisiwani Pemba, Ghassan (2006) anaueleza utani kuwa ni amali muhimu katika jamii na inapotendeka inaondoa dhana ya kuwa utani ni kitu cha kukibeza. Hata hivyo, mara nyingi watani wanapokutana hutanihana kwa maneno huku wakizingatia ma sharti yaundayo uhusiano wao wa kiutani kama vile bibi na wajukuu zake, shemeji na shemeji na mfano wa hayo kwani bila ya mazingatio unaweza kujikuta umemtania mtu asiyekustahikia na kwa muktadha huo sasa utakuwa umemtusi. Kwa mfano, si jambo la kushangaza kuona watu wakifanya utani wakati wa msiba kama Ghassani anavyosema;

Kwa Wapemba utani ni kejeli katika maisha. Watu huko hutanihana wakati wa uzazi na wakati wa matanga. Ni jambo la kawaida sana kumuona mtu katika mkusanyiko wa matanga wakati wengine wanalia yeye amejivisha kanzu na koti la marehemu anamuigiza mwendo wake au sauti yake. Si kuwa hawaumizwi na msiba huo, lakini utani huu ni katika kuyapa maana halisi maisha yao na kuzifunika huzuni zao. (uk.3)

Hivyo, utani unaweza kuwakutanisha watu katika matukio na miktadha ambayo kwa namna moja au nyengine hujenga upendo na kuondosha chuki zilizokwisha jengeka mionganoni mwa wanajamii. Hapo hapo, anaonesha jinsi kejeli na dhihaka itumiwavyo na watu mbali mbali wawe matajiri au masikini. Hapa, mwandishi anaizungumza hali ya wapemba baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 1995 ambapo watu walipigwa ovyo, chakula kilikuwa adimu na kulikuwa na uhaba wa mvua. Waliita sembe nkapa, askari waliitwa melody na njaa iliitwa Komando. Anaendelea

kusema kwamba labda unawenza kufikiria watu wako kwenye hali ngumu kama hiyo na bado wanadiriki kujenga kejeli na tashtiti za namna hiyo. Ndiyo kusema kwamba hiyo ni sehemu ya maisha yao ambayo yana ugumu usiomithilika. Kwao utani ni kibwagizo cha maisha ndio kusema kwamba utani ni kibwagizo cha ugumu wa maisha, hutani na kukejeli ili kujifaraji na kujipumbaza na dhiki iwaandamayo kila uchao. Lakini pia kuutapika ukweli mchungu

BAKIZA (2008) Wanaeleza katika kitabu chao cha *Utamaduni wa Mzanzibari* kwamba Wazanzibari wana desturi ya kufanyiana utani. Kama vile kuitana majina ya utani ambayo huwa maarufu hadi kufikia lile la mwanzo kusahaulika. Wanaongeza kwamba mfano mzuri wa utendekaji wa utani wa Wazanzibari huonekana wakati wa harusi. Watani wa uzawa wa mwanamke anaeolewa humkimbiza harusi asiolewe au mume asioe. Wengine huukamata mkono wa muozeshaji na kudai aozeshwe yeye. Hufanya hivyo mpaka apewe pesa kidogo na ndipo aondoke na kuacha shughuli iendelee. Madhumuni ya kufanya hivyo ni kujitambulisha kuwa yeye ni shemegi yake au mtu wa karibu katika familia. Hapa tunapata taswira kuwa jamii ya Wazanzibari inaikubali jadi hii ya utani katika sehemu mbalimbali na hivyo kuweza kuchunguza athari ya jadi hii kwa watumiaji wa soko na diko.

Iddi (2005), katika tasnifu yake kuhusu “Utani katika Jamii ya Wazanzibari” amezungumzia zaidi nyimbo za utani ambazo huibwa kwenye harusi. Nyimbo hizo ambazo huwa ni za utani, kwa kimantiki ni zenye kutoa mafunzo kwa maharusi. Pia ameeleza kwamba, katika shughuli za Wazanzibari watani ndio husinga maharusi. Pamoja na hayo wakati wa kusingwa utani hutawala. Hii ni kwa sababu mara nyingi shughuli kama hii hufanywa na wale watu unaoweza kuwaowa kwa upande wa

mwanamme, na watoto wa kike wa mjomba, shangazi na madada kwa upande wa harusi mwanamke.

Naye Mkubwa (2012) alifanya utafiti juu ya “Dhima za Utani Katika Maziko na Matanga ya Wapemba na Athari Zake kwa Jamii”. Katika utafiti wake huo alieleza kwamba, utani katika maziko ya wapemba umeanza kuondoka kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo jamii imekuwa ikitekeleza utani katika matanga na dhima yake kubwa ni kujiliwaza baada ya machunu ya kuondokewa. Aidha alifafanua kuwa imani ya dini ya Kiislamu imekuwa ikinasibishwa na kupinga utani katika maziko hasa kwa baadhi ya madhehebu.

#### **2.4 Mapengo ya Utafiti**

Kipengele kuhusu utani kimefanyiwa tafiti mbalimbali, tafiti nyingi zimeshughulikiwa katika kuangalia utani kwa muktadha unaofanana. Hivyo, mtafiti amegundua mapengo yafuatayo: Mosi, tafiti nyingi zimefanywa upande wa Tanzania Bara huku zikijiegemeza zaidi katika utani wa makabila. Hata hivyo zipo tafiti chache zilizofanywa kwa upande wa visiwani ambazo zimeuangalia utani kwa ujumla wake, na baadhi zimejikita katika isimu. Pili, tafiti nyingi zimeangalia utani unaotendeka kwa matukio fulani bila ya kuonesha athari zake. Hivyo, mtafiti anaziba pengo hili kwa kuangalia athari za utani wa sokoni na dikoni kwa kuzingatia kwamba sehemu hizi hutendeka utani kila uchao na kuhusisha watu wanaotoka katika jamii tofauti na jinsia tofauti.

#### **2.5 Hitimisho**

Sura hii imeeleza juu ya maandiko mbalimbali yanayolandana na utafiti huu. Utafiti uliangalia maandiko yanayoueleza utani kwa ujumla wake, na sehemu ya pili

iliangalia maandiko yanayofafanua utani kwa kuangalia mazingira ya Zanzibar pekee. Aidha sura hii ilifikia tamati kwa kuonesha mapengo yaliyoachwa wazi na watafiti waliopita ambayo ndio yaliyotoa nafasi kwa utafiti kuangalia utani katika uga huu wa sokoni na dikoni. Sura inayofuata itaangalia juu ya usanifu na mbinu za utafiti.

## **SURA YA TATU**

### **USANIFU NA MBINU ZA UTAFITI**

#### **3.1 Utangulizi**

Sura hii inafafanua mbinu za utafiti zilizotumika, kwa jumla, ilihuisha mpango wa utafiti, eneo la utafiti, ya watafitiwa, mbinu za kukusanya data, uhalali na uthabiti wa data pamoja na mbinu za uchanganuzi wa data.

#### **3.2 Mpango wa Utafiti**

Utafiti huu ulikuwa ni wa kitaamuli kwani ulionekana kuwa faafu zaidi kwa vile ulitumia njia ya maelezo katika uchambuzi wa data. Pia ulifanyika uwandani na maktabani. Mtafiti alitumia njia ya uwandani zaidi kuliko maktabani kutokana na uhalisia wa utafiti wenyewe. Hii ni kwa sababu wahojiwa wametawanyika sehemu mbalimbali kama vile sokoni na dikoni ambako inaonekana utani unatendeka zaidi. Utafiti huu pia uliongozwa na nadharia ya utambulisho ambayo ililingana na utafiti huu.

#### **3.3 Eneo la Utafiti**

Utafiti huu ulifanyika katika eneo la mjini katika soko la Mwanakwerekwe, Magharibi mwa Mji wa Zanzibar na katika diko la Maruhubi, mjini Zanzibar. Eneo hili liliteuliwa kwa kuangalia vigezo thabiti ambavyo upatikanaji data utakuwa na urahisi. Katika sehemu hizi mkusanyiko wa watu kwa siku ni mkubwa mno na mwingiliano wa watu ni mkubwa jambo linalosababisha utendekaji wa utani kuchukua nafasi kubwa katika sehemu hizo.

### **3.4 Walengwa wa Utafiti**

Walengwa wa utafiti huu wamegawanyika katika maeneo makuu mawili ambayo ni jamii ya watafitiwa na sampuli ya utafiti.

#### **3.4.1 Jamii ya Watafitiwa**

Walengwa wa utafiti huu walikuwa watumiaji wa soko la Mwanakwerekwe Magharibi ya mji wa Zanzibar na watumiaji wa diko la Maruhubi Mjini Zanzibar.

Walengwa hawa wamechaguliwa kutokana na uzoefu kwamba sehemu hizo zina upekee wa utani kulingana na kushiriki watu wa makundi yote katika kupata huduma au ajira kila siku. Jamii iliyotafitiwa ilijumuisha makundi yafuatayo:

- a) Madalali kutoka sehemu zote mbili sokoni na dikoni;
- b) Wachuuzi, wanawake na wanaume, wanaonunua kitoweo katika diko la Maruhubi;
- c) Wanunuzi wa kawaida katika diko la Maruhubi na soko la Mwanakwerekwe Zanzibar;
- d) Wauzaji wa bidhaa mbalimbali katika soko la Mwanakwerekwe Zanzibar;
- e) Wataalamu mbalimbali wa fasihi kutoka Chuo Kikuu cha Taifa SUZA na BAKIZA na;
- f) Wapishi wa dagaa na wabebaji wa dagaa kutoka katika boti katika diko la Maruhubi.

#### **3.4.2 Usampulishaji na Sampuli Iliyotumika**

Kwa mujibu wa Kothari (2003), sampuli nzuri ni ile iliyio ndogo, jumui na itakayomuwezesha mtafiti kuidhibiti. Kombo (2006) anasema: “Kusampulisha ni mchakato wa kuchaguwa idadi ya wawakilishi wenye tabia sawa na walengwa wa utafiti.” Katika utafiti huu, sampuli ilichaguliwa kwa kuzingatia mbinu ya sampuli

lengwa ili kupata uwakilishi halisi. Idadi kamili ya watafitiwa ilikuwa kuwa ni watu 100 kutoka katika makundi mbalimbali ya watu yanayofanya shughuli zao katika soko la Mwanakwerekwe na diko la Maruhubi mjini Zanzibar. Hii ni kwa sababu idadi inategemewa kuwa ya kutosha kabisa kutoa maelezo ya kuwakilisha kundi lote kutokana na utafiti unaotarajiwa kufanywa. Kwa hiyo, sampuli ni hii ifuatavyo:-

- a) Madalali 10 kutoka sehemu zote mbili sokoni na dikoni;
- b) Wachuuzi 30 wanaonunua kitoweo katika diko la Maruhubi;
- c) Wanunuzi wa kawaida 30 wanaopatiwa huduma katika diko la Maruhubi na soko la Mwanakwerekwe Zanzibar;
- d) Wauzaji 20 wa bidhaa mbalimbali katika soko la Mwanakwerekwe Zanzibar na;
- e) Wataalamu 5 wa fasihi kutoka Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) na BAKIZA na wabebaji 5 wa dagaa kutoka katika boti katika diko la Maruhubi Zanzibar.

### **3.5 Ukusanyaji wa Data**

Kipengele hiki kinalezea njia na zana mbalimbali zitakazotumika kukusanya data; pamoja na mchakato wenyewe wa ukusanyaji wa data. Williman (2011:97) anabainisha njia za ukusanyaji wa data kuwa ni mahojiano, hojaji, ushuhudiaji na kufanya majaribio.

#### **3.5.1 Njia zilizotumika Wakati wa Kukusanya Data**

Mtafiti alitumia data za awali kuititia njia ya usaili, ushuhudiaji, na udodosaji Mbinu hizi zinaufanya utafiti huu kuwa halisi zaidi kwani mtafiti alipata kushiriki kikamilifu katika shughuli za utani zifanyikazo sokoni na dikoni.

### **3.5.1.1 Usaili**

Mtafiti alitumia mbinu ya usaili kwa watumiaji wa soko na diko wasio na uwezo wa kusoma wala kuandika. Mbinu hii ilimsaidia mtafiti kubadilishana mawazo na watafitiwa ana kwa ana, ili kuweza kupata undani juu ya mada husika. Pia ilimrahisishia kuweza kuwahoji wale ambao kwa asili ya kazi yao ni vigumu kujaza dodoso. Kwa kutumia mbinu hii mtafiti aliweza kupata mchanganuo mzuri wa taarifa.

### **3.5.1.2 Udodosaji**

Mtafiti alitumia dodoso wakati wa kukusanya data, dodoso zilitumika kwa wale wenye uwezo wa kusoma na kuandika, mbinu hii ilitumika kuwadodosa wataalamu wa fasihi ili kupata maoni na mawazo yao kuhusu utafiti huu. Mtafiti alipata fursa ya kuwadodosa wakufunzi wa somo la Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) na wataalamu wa fasihi ya Kiswahili kutoka Baraza la Kiswahili Zanzibar.

### **3.5.1.3 Ushuhudiaji**

Mbinu hii ilitumika kukusanya data zilizo katika hali ya asili. Nunan (1992) na Adowel (1984) wanaeleza kwamba ili kugundua tabia fulani, mtafiti hana budi kuichunguza katika mazingira ya utokeaji wake. Mtafiti alitembelea sokoni na dikoni ili aweze kugundua namna utani unavyofanyika ili aweze kupata kuangalia tabia ya utani wa sokoni na dikoni. Mtafiti alihudhuria kwenye minada ya nazi nandizi kwa sokoni, na mnada wa samaki kwa dikoni. Njia hii ilimsaidia mtafiti kupata taarifa sahihi na kupata ladha ya jinsi utani unavyotendwa na watumiaji wa sokoni na dikoni.

### **3.5.1.4 Udurusu wa Machapisho Maktabani**

Katika utafiti huu mtafiti alitembelea maktaba mbalimbali kama vile Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA), na maktaba ya Makavazi Chuo Kikuu cha Dar es salaam. Mtafiti alisoma vitabu na majorida mbalimbali ili kupata maarifa na taarifa muhimu zinazolandana na mada ya utafiti huu.

### **3.5.2 Zana Zilizotumika Wakati wa Ukusanyaji wa Data**

Katika ukusanyaji wa data, zana mbalimbali zilitumika katika kukusanya taarifa za utafiti huu na kuzihifadhi. Vifaa kama vile vijidaftari, kalamu, kamera, simu na ngamizi vilitumika. Kamera ilitumiwa na mtafiti kupigia picha sehemu ambazo ziliwa zikitendeka utani hasa wakati wa ushuhudiaji. Pia, mtafiti alitumia vijidaftari na kalamu katika ukusanyaji wa data, ili kuandika taarifa muhimu zinazohusiana na utafiti na kutunza kumbukumbu muhimu kutoka kwa wasailiwa. Ngamizi ilitumika katika kuchapa na kuangalia baadhi ya taarifa katika tovuti mbali mbali zinazohusina na utafiti huu tokea katika hatua za awali. Aidha mtafiti alitumia simu kwani iliweza kuchukuwa nafasi nyingi katika ukusanyaji wa data. Mosi, ni kwa ajili ya mawasiliano; pili, ni kwa ajili ya kurekodi mambo ambayo mtafiti alihisi ni vyema kuyapata kama yalivyo simuliwa wakati wa usaili au ushuhudiaji.

### **3.6 Mchakato wa Ukusanyaji Data na Udhhibit wake**

Utafiti huu ulifuata taratibu sahihi zipaswazo kufuatwa na mtafiti. Mtafiti aliomba ridhaa kwa uongozi wa Chuo Kikuu cha Dodoma; pamoja na kupata kibali kutika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar ambaye ndiye mtoa idhini kisheria kwa upande wa Tanzania Visiwani ili kupata uhalali wa kuingia sehemu mbalimbali kukusanya data. Aidha, tahadhari ilichukuliwa katika kuhakikisha kuwa taarifa zote zinazotoka kwa wahojiwa zinakuwa siri. Data za uwandani zilikusanywa kwa njia ya

usaili, dodoso na ushuhudiaji. Mwongozo wa usaili ulitumika kuwahoji watumiaji wa soko la Mwanakwerekwe na diko la Maruhubi mjini Zanzibar, dodoso lilitumika kuwahoji wataalamu wa fasihi ama njia ya ushuhudiaji itatumika kwa mtafiti kutembelea soko na diko ili kuona utendekaji wa utani katika sehemu hizo.

### **3.7 Uchambuzi wa Data**

Uchambuzi wa data za utafiti huu ulizingatia nadharia ya Utambulisho wa Jamii. Data zimechambuliwa na kupangwa kulingana na malengo ya utafiti wetu. Hivyo, kila lengo limejijengea hoja kulingana na maudhui husika. Mbinu ya ufanuzi imetumiwa katika kuchambua data kwa sababu data za utafiti huu zimetiririka kwa maelezo. Data zilizopatikana uwandani kwa kutumia madodoso, usaili na ushuhudiaji ziliwasilishwa sambamba na zile chache za maktabani ili kutoa matokeo halisi na yanayowiana.

### **3.8 Mipaka ya Utafiti**

Utafiti huu uliangalia nafasi ya utani kama utanzu wa fasihi simulizi. Aidha, utafiti ulishughulikia maeneo yenyeye mkusanyiko wa kila siku ambao wanajamii hupata huduma zao za kila siku hasa sokoni na dikoni.

### **3.9 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi Wake**

Mtafiti alikabiliana na vikwazo kama vile uhaba wa fedha kwa ajili ya ufamiliaji wa maeneo ya kukusanya data. Baadhi ya wahojiva kutokua tayari kutoa majibu ya maswali ya mtafiti, wakidhani kuwa ni upuuzi na kuwapotezea muda wao. Kwa upande wa sokoni ilikuwa ni vigumu kutiririka na mahojiano bila ya kukatisha njiani, kwa vile mara wateja walikuwa wakitaka kupatiwa huduma. Hata hivyo, mtafiti alitafuta sehemu na kuwaomba aliyekuwa na nafasi aje nimsaili na hatimae

kuendelea na kazi yake. Mtafiti pia alipata usumbufu kwenye kutafuta data za maktabani kwani hakuna vitabu vingi vinavyozungumzi utanzu huu wa utani moja kwa moja. Katika kukabiliana na matatizo hayo mtafiti alifanya maarifa ya kufinya matumizi na hata kukopa kwa jamaa wa karibu pale ilipobidi. Ama kwa upande wa vitabu mtafiti alijaribu kuangalia kwenye mtandao ili kupata muongozo zaidi.

### **3.10 Hitimisho**

Sura hii imefafanua kuhusu mbinu na vifaa vya utafiti vilivyotumika katika utafiti huu. Mbinu zilizotumika zimefanuliwa ili kukidhi haja ya mazingira na mada ya utafiti huu. Zana za kukusanya data zilienda sambamba na watafitiwa walioteuliwa. Mahojiano udodosaji na ushuhudiaji zilitumika katika kupata data kutoka kwa jamii ya watafitiwa ambayo iliteuliwa mahsus i kufanikisha utafiti huu. Njia na mbinu hizi zilimrahisishia mtafiti kufanya kazi zake kwa ufanisi. Aidha sura tunayoielekea inazungumzia uwasilishaji, uchambuzi na matokeo ya utafiti.

## **SURA YA NNE**

### **UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MATOKEO YA MJADALA WA UTAFITI**

#### **4.1 Utangulizi**

Sura hii inajadili kwa kina matokeo ya utafiti. Mjadala huo umegawanyanya katika sehemu kuu tatu kwa kuzingatia maswali na malengo ya utafiti huu. Sehemu ya kwanza inafafanua sababu zinazochangia kuzuka kwa utani wa sokoni na dikoni kwa jamii ya Wazanzibari. Pili, inabainisha muundo wa utani wa sokoni na dikoni kwa jamii ya Wazanzibari; na hatimaye, inajadili athari za utendekaji utani jinsi zinavyohusiana na utamaduni wa Mzanzibari. Hivyo, katika kila sehemu ya sura data zimewasilishwa kwa njia ya maelezo na kuongozwa na nadharia ya Utambulisho wa Jamii ambayo msingi wake ni wanadamu walivyojijengea silka ya kupenda kujitambulisha na kundi au jamii inayohusiana nayo, kulingana na walivyo, sehemu ya kundi au jamii na kujitambulisha kama kundi jengine.

#### **4.2 Taarifa kwa ufupi kuhusu Wazanzibari**

Hapa mtafiti anaelezea kwa ufupi miktadha mbalimbali inayoizunguka jamii ya wazanzibari katika maisha yao ya kila siku. Taarifa hii itatupa muonekano kamili wa Zanzibar kijografia, kiuchumi na kiutamaduni ili kuelwa uhusiano wao jadi hii ya fasihi simuliza katika kipengele cha utani.

##### **4.2.1 Miktadha ya Maisha ya Wazanzibari**

Zanzibar ni mkusanyiko wa visiwa viwili vikubwa, navyo ni Unguja na Pemba. Vipo visiwa vingine vidogo vidogo kama vile Chumbe, Tumbatu, Fundo, Kisiwa Panza, Kojani, Changuu, Bawe na Uzi. Tangu karne na karne mchanganyiko wa utamaduni ndipo ulioipa sura Zanzibar ya leo. Wasyiria, Wapersia, Wamisri, Wahindi,

Wachina, Wareno, Waarabu wa Omani, Wadachi, Waingereza na wageni wengine waliishi kwa nyakati tofauti na wenyeji wao Waafrika. Hivyo kusababisha muingiliano wa damu na tamaduni.

#### **4.2.1.1 Muktadha wa Kijografia**

Zanzibar inaundwa na visiwa ambavyo vimetenganishwa na bahari. Kijografia, kidogo vinatofautiana kwani, kisiwa cha Pemba kina miinuko zaidi ya kile cha Unguja. Kisiwa cha Unguja kiko umbali wa km 40 kutoka Tanzania Bara Mashariki mwa Bagamoyo. Na kisiwa cha Pemba kinapatikana umbali wa kilomita 50, Kaskazini mwa kisiwa cha Unguja. Zanzibar inapatikana kwenye nyuzi  $6^{\circ}$  Kusini mwa Ikweta. Ina urefu wa km 85 na upana wa km 35. Ina ukubwa wa eneo la kilomita za mraba  $14560 \text{ km}^2$  za kisiwa cha Unguja na  $985 \text{ km}^2$  kwa kisiwa cha Pemba. Hivi ni visiwa vyenye mikoa mitano, ambapo Pemba kuna mikoa miwili na Unguja mikoa mitatu. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012, visiwa hivi vina wakaazi takriban milioni moja na laki tatu.

#### **4.2.1.2 Muktadha wa Kiuchumi**

Kiuchumi, Zanzibar inategemea zaidi kilimo, ufugaji, uvuvi na utalii. Kwa upande wa kilimo Wazanzibari hujishughulisha na kilimo cha mazao makuu ambayo ni karafuu, nazi na mwani ambayo ni mazao ya biashara. Pia, hulima mazao ya chakula kama mihogo, mpunga viazi, migomba, na mazao ya viungo kama vile pilipili hoho, iliki, mdalasini na pilipili manga. Kilimo kinachangia pato la taifa kwa asilimia 27.9% hasa kupitia zao la karafuu. Kuanzia miaka ya themanini Wazanzibari walijishughulisha na kilimo cha mwani. Kilimo hiki huzalishwa pwani, ambapo baadaye huvunwa na kuanikwa kwa ajili ya kusafirisha ng'ambo kama vile Ulaya na Asia. Hata hivyo, Zanzibar huagiza nje bidhaa kama vile mchele, mafuta ya kupikia,

mahindi, sukari na unga wa ngano. Shughuli za ufugaji huhusisha ufugaji wa ngombe, mbuzi, kuku, na samaki nao umesaidia kuinua kipato hasa kwa watu wa vijijini. Kwa vile visiwa hivi vimezungukwa na bahari wakaazi wake kadhalika hujishughulisha na uvuvi, mionganoni mwa shughuli zao ni kuvua samaki, pweza, kombe, kamba na aina nyengine za vitoweo. Aidha, sekta ya utalii imekuwa ikichangia pato la taifa kwa asilimia kubwa. Hii ni kutokana na kwamba Zanzibar ina vivutio vingi vya utalii kama vile fukwe maridhawa, sehemu za kihistoria na hali ya hewa.

#### **4.2.1.3 Muktadha wa Kiutamaduni**

Kiutamaduni, watu wa Zanzibar wanatofautiana na maeneo mengine ya Tanzania hususani katika mapishi, mavazi, pamoja na namna ya kushughulikia misiba na sherehe za harusi. Kwa Wazanzibari Kiswahili si kwamba ni lugha ya Taifa tu, bali pia ni lugha yao ya kwanza. Hata hivyo, kuna lahaja tofauti zinazozungumzwa kama vile, Kitumbatu, Kimakunduchi, Kipemba na Kiunguja mjini.

Asilimia kubwa ya wakaazi wake ni waumini wa dini ya Uislamu. Hali hii huzifanya mila na desturi zao ziendane na dini ya Kiislamu. Utamaduni huo ni zao la muingiliano kati ya wenyiji na wageni waliofika Zanzibar katika nyakati tofauti na kwa madhumuni mbalimbali. Kwa upande wa mavazi, watu wa Zanzibar hupendelea kucaa nguo kama vile kanzu, kofia, seruni, kikoi, kilemba, suruali na shati kwa wanaume. Ama kwa upande wa wanawake, hujisitiri kwa mavazi kama vile buibui, mtandio, kitenge, kanga, mashungi (hijaab) na kanzu. Lodhi (1999) anaeleza kuwa, kutokana na kuwa Zanzibar ipo katika bahari ya Hindi upwa wa Afrika Mashariki, iliweza kupata wageni kutoka Uarabuni, India, China na nchi za Ulaya. Wageni hao waliingia Zanzibar kwa shughuli tofauti zikiwemo za kibashara. Mwishowe

wachache walioa na kuolewa na kuwa wakaazi wa kudumu wa sehemu hizi. Hivyo, Zanzibar ikapata kuwa na utamaduni wa mseto. Watu hao wamejenga silka, mila na desturi tofauti muingiliano wa tamaduni tofauti, mionganini mwa mila na desturi zilizojengwa ni utani.

#### **4.2.2 Sababu za Kuzuka kwa Utani wa Sokoni na Dikoni Kwa Jamii ya Wazanzibari**

Dhana ya utani kwa jamii ya Wazanzibari si ngeni masikioni mwa walio wengi. Hata hivyo, kwa muktadha wa kuifahamu kama ni kipengelele cha fasihi ni ngeni hasa kwa wale wasiosoma elimu ya darasani. Katika kuibua dhana hii kinadharia na kimatendo utafiti umeibua sababu zifuatazo zinazosababisha kuzuka kwa utani katika maeneo ya masoko na madiko.

##### **4.2.2.1 Uhusiano wa Kibiashara kwa Watumiaji na Soko na Diko**

Utafiti ulibaini kuwa, sokoni na dikoni ni sehemu zenye muingiliano mkubwa na watu, ambao hukutana takribani kila siku. Mara nyingi makundi ya watu wanaoingia na kutoka kwa siku ni yale yale. Hivyo, suala la utani kwa Wazanzibari wafanyao shughuli zao sokoni na dikoni halina tarehe maalum ya kuzuka kwake; bali, ni urithi kutoka kwa babu zao. Mkusanyiko wa watu uliopo katika sehemu hizi hauwezi kunoga pasi na malumbano ya utani. Hii ni kwa sababu ndio chachu ya kupeleka mbele shughuli za kazi zinazofanywa na watu katika maeneo haya. Kwa vile sehemu hizi zinahudumia mamia ya watu kwa wakati mmoja, si rahisi watu wote kuwa na mahusiano ya kiutani isipokuwa kunakuwa na utani baina ya kikundi na kikundi au baina ya mtu mmoja na mtu na mtu mwengine. Kwa mfano, kundi la madalali wa nyanya kuwatania wauza nyanya au mbebaji mizigo akamtania muuzaji kwa upande wa sokoni. Ama kwa upande wa dikoni utani unaweza kufanywa kati ya wavuvi na

madalali, wabebaji dagaa na wavuvi, na waanikaji na tajiri. Ukichunguza kwa kina maeneo na umbali wa sehemu watokazo watu hawa utakuta kuwa ni uhusiano wa kukutana kila uchao katika shughuli zao za kujitafutia riziki. Muktadha huu husababisha kuzuka utani pasi na kujuana kwa kutoka sehemu moja; bali kwa mahusiano waliyonayo kibiashara. Hivyo basi, msingi wanadharia ya Utambulisho wa Jamii unaozungumzia matabaka na mgawanyiko katika jamii huonekana kuwasukuma wanajamii kuamua kwa hiari zao kuwa na mahusiano ya kiutani kwa kuzingatia uhuru wa kuamua kuwa na mtani anayelandana naye bila kutokea mizozo.

#### **4.2.2.2 Uhusiano wa Kiukoo**

Katika matukio kama vile ya harusi na misiba, utani hutegemea zaidi uhusiano ama wa kikabila au wa kiukoo kama vile mashemeji, binamu, na bibi au babu na wajukuu zake. Katika muktadha wa sokoni na dikoni, uhusiano wa kiukoo unasababisha kuzuka kwa utani kwa kiasi. Utafiti ulionesha kuwa mtani anapokwenda kupata huduma sokoni au dikoni na kumkuta shemeji yake au binamu yake hakuna sababu itakayowazuia wasitaniane kwani, wao tokea asili ni watani. Aidha, malumbano ya kiutani kati ya watu hawa yanaweza yakachanganyika kati ya maongezi yahusuyo mandhari ya sokoni au dikoni, na papo hapo yanaweza kutokea mengi yanayohusu mambo ya matukio ya kifamilia. Hii ilitokea pale muhusika alipojiwa na shemeji yake katika soko na kutaniana kama:-

Mfanyabiashara: “assalam alaykum.”

Shemeji:” waalaykum salaam.”

Mfanyabiashara: “haya sema bibie nikuhudumie.”

Shemeji: “nataka viungo vya mchuzi bwana we! Leo nimeona nije mwenyewe niwaone hao wanaokushughulisha.”

Mfanyabiashara: “Nathubutu kuwa na mwengine na ndugu yako kaniweza!”

Katika majibzano haya ilithibitika kuwa utani wa kiukoo waweza kuwa na uhai popote pale ambapo wahusika watakutana bila ya kujali hadhira iliyowazunguka. Kwa mnasaba wa nadharia ya utambulisho wa jamii hapa wahusika hujitambulisha kuwa wao ni watu wa familia moja.

#### **4.2.2.3 Kutambulisha Kazi Anayoifanya**

Utafiti huu umebaini kuwa, shughuli zifanywazo sokoni na dikoni si za aina moja kwa watu wote. Watu hutofautiana kikazi kwa mujibu wa uwezo wao kifedha na kimwili. Katika mandhari ya sokoni kuna watu wanaonadi bidhaa (madalali), mama ntilie, wauzaji maduka, wauzaji samaki, nyama, viungo, wasafishaji na shughuli nyingine nyingi. Ama kwa upande wa dikoni tunawakuta wavuvi, mafundi wa majahazi, wachuuzi, waanikaji dagaa, wabebaji dagaa, wapishi na madalali. Utani humtambulisha mtu kazi anayoifanya, Kwa mfano, dalali wa dikoni au wa sokoni kazi yake ni kuthaminisha bidhaa kwa mujibu wa maelekezo ya wenye mali. Katika shughuli yake hiyo, utani ndio unaomvutia mnunuzi wa bidhaa ile kutokana na bashasha na haiba ya mtu yule. Ucheshi wake ndio unaomtambulisha yeye anafanya nini na kuwavuta matajiri kuwatafuta na kuwapatia kazi kila siku. Katika muktadha huu matamshi ya watani hutofautiana kulingana na shughuli husika. Ni vigumu kwa mama ntilie kufanya utani anaoufanya dalali au mbeba mizigo. Hali hii hulandana na Utambulisho wa Jamii na kuakisi msingi wa ulinganishi katika jamii ambapo mtu huvutiwa na mtu au kundi la watu na kuiga matendo wayafanyayo kulingana na mila na desturi zilzopo.

#### **4.2.2.4 Ugumu wa Kazi Wanazozifanya**

Utafiti uligundua kwamba, mionganoni mwa sababu zinazowafanya watu wataniane katika mjumuiko wa masoko na madiko ni ugumu wa kazi wanazozifanya. Hali ya

majukumu waliyonayo viumbe hawa katika shughuli zao za kila siku zilionekana kuhitajika kwa liwazo la nafsi zao. Kwa mfano, wabebaji wa dagaa hufuata jahazi umbali wa kilomita moja kutoka kwenye fukwe, ikiwa maji yametoka. Kutokana na ugumu wa maisha baadhi ya wanawake wa Ki-zanzibari wamekuwa wakishughulika na shughuli hizi. Hivyo, utani huchukua nafasi yake kuwa kama ponyo la machungu wanayoyapata na hatimae kujikuta wakifanya kazi kubwa na nzito lakini hawakuchoka sana. Zaidi ya hayo, utafiti umebaini kwamba baadhi ya watu wanaweza kutoka nyumbani wamekasirika lakini, wakifika sokoni au dikoni na kutaniana basi husahau machungu yale na kurudi nyumbani wakiwa wako sawa. Hoja hii inathibitishwa zaidi na Mzee Chai<sup>1</sup> kwamba; hata Rais wa kwanza wa Zanzibar, Marehemu Mzee Abeid Karume, alikuwa akifika dikoni kwa kufata watani wake pindi inapomjia hamu yaku kuonana na wale mabaharia wenziwe.

#### **4.3 Muundo wa Utani wa Sokoni na Dikoni**

Utafiti ulibaini kuwa, utani wa sokoni unaundwa kwa kuzingatia miundo ya aina mbili. Kwanza, ni utani wa maneno na pili, ni utani wa matendo. Utani wa maneno katika mandhari ya sokoni hutawala zaidi muda wa shughuli za sokoni au dikoni zikiendelea. Maneno hayo hutamkwa kwa madhumuni ya kuchekesha, kuliwaza, kupunguza machungu na kuvuta wateja. Aidha, pamoja na maneno hayo kuwa ya dharau, kejeli na dhhaka, bado wahusika huyatumia bila ya kuleta athari yoyote mbaya. Ama maneno kama hayo, yatakapotumiwa na mtu kumwambia mtu ambaye kikawaida si mtani wake, au alishatowa tahadhari kuwa hataki kutaniwa yanaweza kusababisha athari mbaya kwa wahusika. Utafiti uligundua kwamba, ndani ya maneno ambayo watani hutupiana kimasikhara, mnawenza kukuza furaha ucheshi na

---

<sup>1</sup> Mzee chai ni fundi wa majahazi katika diko la Maruhubi. Mahojiano yake na mtafiti yalifanyika huko tarehe 22/12/2014

tabasamu ambalo linaweza kuonekana kwa mtaniwa na mtani pamoja na hadhira inayowazunguka. Mtindo huo wa kurushiana maneno uligundulika kuwa hauna kanuni ya kufuatwa, isipokuwa ni utashi na muktadha wa wale watanianao na uwezo wao wa kuvumiliana.

Aina ya pili ni utani wa matendo ambao kwa mazingira ya sokoni au dikoni hutumika lakini ni kwa kiasi kidogo. Utafiti ulionesha kwamba, utani wa matendo huchukuliwa zaidi na mwelekeo wa matusi, na kukashifiana. Ponera (2014) anasherehesha utumiaji wa matusi katika utani kwa kusema kwamba: hiki ni kipengele cha muhimu katika uhusiano wa kiutani ambapo watanianao huweza kufanya mahusiano ya kuhabarishana, kuonyana au kuelimishana kwa kutumia lugha yenye matusi. Watu wengi hawapendelei utani wa matendo ingawa hufanywa na baadhi yao katika mandhari ya sokoni na dikoni. Mtu anaweza kumshika mwenziwe kiuno kwa kutaka kupigana au kutekenya. Utafiti ulionesha kuwa utani wa matendo mara nyingi hufanywa kwa kumuangalia mtu mwenyewe alivyojiweka na anavyojiheshimu. Utafiti ulibaini kuwa aina hii ya muundo wa utani haina waumini wengi, kwani Wazanzibari hufungwa na mitazamo ya dini ya Kiislamu ambayo huweka mipaka ya kutaniana hasa kwa kigezo cha jinsia. Aidha silka na huluka zao zimekuwa zikizisuta nafsi kupunguza baadhi ya mambo ambayo yanavua haiba na heshima ya Mzanzibari.

#### **4.3.1 Sampuli za Matukio ya Utani wa Sokoni na Dikoni**

Utani wa sokoni na dikoni ni utani ambao hutambwa na kunenwa katika matukio mbalimbali. Matukio hayo hutendwa bila kupangiwa muda maalum wa utokeaji wake. Lifuatatalo nitukio la kwanza la utani ambalo lilishuhudiwa katika mnada wa nazi:

Dalali: *Anaanza kwa kushitua kwa kelele*“Eheeee! Wale wateja wa nazi za kuanguka nnazo hapa! Haya nauza tonge kwa tonge vibuwa vimo, sehewa wamo, mia tano, mitano thelathini, tano thelathini nambarikia mkulima tano thelathini iyoo!”

Mnunuzi: “Tano thalathini!”

Dalali: “Nampiga nazo kwa mia thelathini au namkanyaga kwa mia tano.”

Mnunuzi: “Fanya mia mbili hamsini.”

Dalali: “Mia mbili hamsini kwa iibiwa (imeibiwa) hiyooo!”

Malumbano haya ya kiutani hufanyika katika mnada wa nazi, ambapo dalali huwa ndiye kiranja mkuu wa shughuli hii. Kwa kawaida, mnada hutawaliwa na kauli za utani. Mathalani, katika tukio la hapo juu, tungo isemayo: “Nampiga nazo kwa mia thelathini au namkanyaga kwa mia tano” imebeba vionjo vyta ya kiutani. Hii ni kwa sababu katika hali ya kawaida, neno kama vile ‘kanyaga’ hutumiwa kwa maana tofauti tofauti. Kiisimu, huweza kumaanisha kumdidimiza au kumkandamiza kwa kutumia mguu. Hata hivyo, huweza kuwa na maana nyingine kadri ya sajili za lugha. Aghalabu, watu wengi hulitumia neno hili kumaanisha tukio la kufanya ngono, hususani ile ya kinyume na maumbile. Miundo ya lugha kama hii ni nadra kusikika ikitumika kwenye hadhara nje ya muktadha wa utani kwa sababu ya hali ya utusi. Lakini, ni jambo linaloonekana kukubalika katika muktadha kama huu wa mnada.

Bashasha na nderemo za dalali huwa ni kichocheo cha kuipeleka siku mbele. Hali hii, kwa mujibu wa nadharia ya Utambulisho wa Jamii hubeba dhima kubwa zifuatazo: Mosi, ni dalali mwenyewe kujibainisha kwa wateja wake kuwa ni mhusika wa zoezi la mnada. Pili, ni kuitambulisha shughuli yake ya mnada (ambayo aghalabu huendeshwa kwa kelele zenye lugha za matusi na utwezaji). Utafiti umebaini kuwa matumizi ya lugha za utani katika mnada huwaondolea wateja hofu ya kununua bidhaa. Hii ni kwa sababu mnunuzi anaweza akavutiwa na bei na

kununua hata kama atakapokuja kuuza atapata hasara lakini mwenye bidhaa yake atakuwa ameshauza.

Tukio jengine ni hili linalohusiana na mazingira ya mnada wa samaki ambapo utani ulijitokeza ni hili lifuatalo:

Dalali: “Haya sema ‘apo! Ngapi na ngapi ngapi na ngapi? ”

Wanunuzi: Hamsini, hamsini na tano, arobaini na tano, ishirini, ishirini!(*Wanunuzi hutaja bei tofauti. Na wengine huweza kuendelea kushusha bei*)

Dalali: “Kampe mkeo hizo.”

Wanunuzi: (Wanaendelea kutoa bei na atakayekuwa katoa bei ya juu kuwashinda wenziwe huambiwa mbarikie huyo hapo sioni).

Dalali: “Nambarikia.”

Dalali: “Nondo hiyoo. Haya ngapi hiyooo!”

Wanunuzi: “Tano hiyo!”

Dalali: “Elfu tano, elfu sita...”

Utani huu hufanyika dikoni mara tu chombo kifikapo na kutia nanga. Wanunuzi husogea karibu kusubiri mnada kwa ajili ya kununua kitoweo na kwenda kuchuuza mitaani. Kikawaida, wavuvi wanapotoka kuvua huwa hawana jukumu la kunadi kitoweo.Tofauti na kwenye mnada wa sokoni, hapa dalali hutia bei na kuwaachia wateja washindane kwa bei. Katika kutafutwa mtu atayeshinda na kubarikiwa wahusika hutupiana maneno ya mzaha ili kuleta ucheshi na kumfanya dalali awe makini kuamua nani abarikiwe. Kwa mfano, mnunuzi anapoweka bei ya chini kuliko thamani ya bidhaa yenewe dalali huweza kusema: “kampe mkeo|” au kuanza kutia bei ya juu kwa kusema: “nondo hiyo!” Matamshi kama haya nje ya utani huonekana kuwa ni kifaa kinachotumiwa katika ujenzi lakini kwa muktadha wa dikoni, neno hili lina maana ya elfu kumi hao! Sambamba na neno ‘kampe mkeo’, katika hali ya nyumbani mtu huweza kuagizwa kwa kuambiwa kitu fulani kampe mkeo na isitokee shida kutegemea na nani amemuamuru kufanya hivyo. Ama kwa upande wa dikoni kauli hii hutumika kubeza na kudharau bei hafifu aliyoitia mnunuzi wakati wa

mnada. Majibizano haya hufanyika kiutani na hata inapotokea kutukana katika muktadha huu basi haichukuliwi kuwa matusi, bali, huchukuliwa ni mambo ya kawaida. Hata hivyo, lugha hizi huishia hapo hapo dikoni na zikitumika nje ya hapo huweza kuleta ugomvi. Lakini ni maneno ya kawaida kwa muktadha wa mnadani. Kwa kutumia nadharia ya utambulisho wa kijamii yenyе msingi unaomtaka mtu kujitambulisha kutokana na vigezo maalumu alivyonavyo mtu, utafiti umebaini kuwa maneno na vitendo hivyo hutumika sokoni ili dalali ajitambulische kwa wanunuzi wake.

Utani mwingine unaojielekeza katika lugha yenyе chembechembe za matusi ulidhihirika katika mazingira ya uchukuzi. Mfano wa kauli za jinsi hii ni huu ufuatao:

“Nipe nyuma!” au  
“Vumba hilo!”

Maneno kama haya huwa ni matusi kwa mazingira yasiyokuwa ya sokoni; bali kwa sokoni hubadilika na kuwa utani. Kauli kama “Nipe nyuma!” ni kauli yenyе mchomo mkali wa matusi, hasa kwa waumini ya dini ya kiislamu. Kwani sehemu hii ya maumbile ni mwiko kutumika kwa maingiliano ya watu, hata walio halali kindoa. Tungo hii, itumikapo katika muktadha wa sokoni hugeuka maana. Kwa mtazamo wa kawaida, mtu aliyeambiwa maneno hayo hupisha njia na kuona ametaniwa tu. Lakini, kwa kutumia misingi ya nadharia ya utambulisho wa kijamii utafiti umebaini kuwa matusi hayo hayatolewi kwa kuomba njia tu, wala kutukana bali mchukuzi huwa anajitambulisha kazi yake kuwa ngumu, na maombi yake yanataka utekelezaji tu yaani upishe njia watu wapite, mara nyingi watu watacheka ila watakupisha haraka. Utafiti umebaini kuwa matumizi ya tungo kama hizi zenye utani ujengwao na matusi husababishwa na aina ya kazi wazifanyazo. Ugumu wa kazi hizo ndiyo husababisha

mtu asipate muda wa kumuomba mtu kwa ustaarabu ampishe. Zaidi ya hilo, matumizi ya tungo hizi za kiutani katika mandhari ya uchukuzi wa mizigo sokoni hupunguza uchovu na kuongeza nguvu ya kazi.

Tukio jengine la kiutani hutokea katika mazingira ya uvuvi kama mfano unavyoonesha hapo chini:

Mvuvi: "We! Mwajuma we! Hebu vuta! Umeregea kiasi hicho!"

Mvuvi 1: "Niletee mkeo uone! Kama sijamzalisha kama panya!"

Mvuvi 2: "We! Ukimuona mke wangu si wewe mwenyewe utajiona mwanamke tu!"

Mvuvi 3: "Jaribu uone kisirani we!"

Mvuvi 4: "Nenda ukakanyagwe we! Mwanamme anakuwa hivyo!"

Katika muktadha wa uvuvini, wavuvi hukaa pamoja na kufanya kazi zao kama vile kushona nyavu, kupika, kusuka madema nakadhalika. Wakati shughuli hizi zikiendelea watani hutupiana maneno ya utani ya hapa na pale. Utafiti uligundua kuwa, utani unaofanywa sehemu hii ni tofauti na sehemu nyingine. Mara nyingi matusi hutawala muda wote wa kazi. Kejeli, dharau na dhihaka huwa ni jambo lililo kama sheria kwao. Hapa, utafiti uligundua kuwa, kauli kama kukanyagwa, kisirani, Mwajuma ni kauli za dhihaka na dharau. Kwani, mwanamme kumwita jina la mwanamke si heshima, halkadhalika kitendo cha kukanyagwa ni kitendo cha kufanyiwa mwanamke na sio mwanamme. Hivyo, kumwambia mwanamme mwenzio akakanyangwe; ni matusi makubwa nje ya hadhira ya uvuvini lakini kwa mazingira ya uvuvini ni lugha ya kawaida. Matusi hayo hayatolewi kwa lengo la kutusi bali huhamasisha kufanya kazi kwa bidii na kuimaliza kwa wakati. Hivyo, wahusika wa sehemu hii hulazimika kuiga lugha hiyo wafikapo dikoni, ili kunasibiana na kundi wanalokabiliana nalo; kama moja kati ya msingi wa nadharia

ya utambulisho inavyoeleza kwamba, mtu mwenyewe anatambua anachoiga kutokana na kuvutiwa na mtu au kundi la watu.

Tukio jengine ni lile lililojitoza katika mnada wa ndizi, nalo ni:

Mnunuzi wa kwanza: “mzee kushafika; naona umewahi?”

Mnunuzi wa pili: “ndio nimeipata ndizi mbili lakini ipo moja inataka kunadiwa.”

Mnunuzi wa kwanza: “Kwa hiyo mimi nimekosa?”

Mnunuzi wa pili: “Si ndizi tu hata kwa mkeo yaonesha kushakosa.”

Mnuzi wa kwanza: basi hii huipati.”

Mnunuzi wa pili: “Acha apige mnada tutie bei.”

Dalali: “eflu sita, elfu sita, elfu sita...”

Mnunuzi wa kwanza: “elfu saba.”

Mnunuzi wa pili: “elfu nane.”

Mnunuzi wa kwanza: “elfu tisa”

Mnunuzi wa pili: “elfu kumi na tatu.”

Mnunuzi wa kwanza: “elfu kumi na tano.”

Dalali: elfu kumi na tano nampiga nazo.

Mnunuzi wa pili: mimi nilikuwa nakuacha utie bei tu nikutie hasara.

Mnunuzi wa kwanza: mimi huwezi kunitia hasara manake spidi ya kutia leo nimeianza kwa mkeo.

Tukio hili, lilihuhudiwa katika mnada wa ndizi, ambapo utafiti ulibaini kuwa utani ni jambo linaloweza kuleta mfarakano usiotabirika endapo wahusika watakosa uvumilivu na subira. Kitendo cha kumwambia mtu ‘nimeianza kutia kwa mkeo’, ni matamshi ya kichochezi ndani na nje ya soko kwani hata kama kauli hii kwa upande wa sokoni hutolewa kiutani, bali, ni watu wachache wanaoweza kustahamili. Pia, tukio hili linatuonesha jinsi tofauti za huluka za watu zisizofichika mbele ya kadamnasi. Mnunuzi wa kwanza ambae alishawahi mnada na kupata ndizi mbili alipaswa kumuachia mwenziwe achukuwe ili iliyobaki lakini, uamuzi wake wa kuitia bei ulikuwa na dhamira ya kumkomowa mnunuzi wa pili kwa kuchelewa kwake, lakini kwa vile utani mara nyingi hubebwa na ukweli, ni dhahiri kuwa mnunuzi wa kwanza alikuwa na lengo la kujinufaisha ye ye pekee.

Katika hali ya kawaida ubishanaji husababisha mapigano jambo ambalo sio jema katika kujenga mahusiano mazuri kwa wafanya biashara. Tukio hilo linaonesha kwamba katika utani wa maneno unaotamalaki kwa watu wa sokoni au dikoni, wahusika wamekuwa wakichukizwa na uhusishaji wa malumbano ya kiutani yanayohusu familia, hasa katika maingiliano ya wanaume na wanawake. Athari ya mwenendo huu wa utani ni kubwa na inakuwa haiondoki moyoni kwa mara moja ilhali machoni inaweza ikarudi katika hali ya kawaida.

Tukio jengine lilijitokeza kwa waanikaji dagaa dikoni kama ifuatavyo:

Muanikaji wa kwanza: “naona kipindi hichi ni cha mvua unachukuwa dagaa?”

Muanikaji wa pili: “mie sichukuwi.”

Muanikaji wa kwanza: “mie ntapigapiga ‘ivo’ivo.”

Muanikaaji wa pili: “sawa.”

Muanikaji wa pili: “hee naona mara hii una mali nzuri. Faida juu kwa juu.”

Muanikaji wa kwanza: “njoo uchukuwe na wewe ukampe mamayo aondowe umasikini.”

Uanikaji dagaa ni shughuli inyofanywa na baadhi ya wakaazi wa mji wa Zanzibar wake kwa waume. Shughuli hii hutegemea bamvuwa lakini ufanisi wa kazi hii huenda sambamba na uwepo wa juwa kali ili kukausha dagaaa hilo. Tukio la utani linalojionesha hapo juu linaonesha jinsi utani ulivyotumika kutoa tahadhari kwa jamii ili iwe makini na ufanyaji wa shughuli zao. Kauli kama: ‘Njoo uchukuwe na wewe ukampe mamayo aondwe umasikini’ ni kauli inayoonesha kutusi na kuvunjiana heshima kwa mujibu wa idili za Wazanzibari. Mama ni kiumbe muhimu kinachohitaji kuenziwa na kuheshimiwa, haijalishi kuwa ni mama mzazi au ni wa mtu mwengine. Pamoja na heshima anayostahili mama kauli hii ilitumika kiutani baada muanikaji wa kwanza kukejeliwa na muanikaji wa pili kwa kutojali ushauri aliopewa wa kuacha kufanya shughuli ya uanikaji wakati wa mvua. Kauli za utani zilizotawala hapo mbali ya kutoa ucheshi kwa hadhira iliowazunguka watu hao, pia,

ilikuwa na lengo la kutambulisha kuwa, jamii ya wafanya biashara hujijengea tabia ya kujipa tamaa ya kupata mafanikio ya kazi zao, kwa mnasaba wa kundi walilo, bila kujali hasara au faida itakayojitokeza mbele yao.

Pia, katika tukio la ushonaji nyavu zipo kauli na matendo ya utani yanazotawala wakati wa kazi hiyo. Miongoni mwa matendo hayo ni:

Mvubi 1: (anakuja mmoja kachelewa) “Ha! Kun’zuiwa ni mkeo mbona kun’chelewa?”

Mvubi wa 2: “wasema sie hatuna wake?”

Mvubi wa kwanza: “hawajuwi mambo hao”

Mvubi wa 3: “hebu njoo ushike yako nyavu huku”

(wanaendelea kushona na kuzikaguwa sehemu zilizobaki)

Mvubi wa 4: “ha! jamaa huyu n’nani aliyeacha tobo wazi utadhani chupi bovu la n’kewe.”

Kikawaida wavuvi huvuwa kwa kutegemea bamvuwa, ambalo hufuatana na muandamo wa mwezi. Mwezi unapon’gaa samaki huwa ni shida kupatikana kwa kile kinachodaiwa kujikusanya sehemu moja. Hivyo, wavuvi hupandisha vyombo na kufanya shughuli nyengine. Miongoni mwa shughuli zifanywazo juu ni kama vile kukalafati vyombo, kushona nyavu, na mambo yahusianayo nayo. Kwamfano, neno “ha! Jamaa huyu n’nani aliyeacha tobo wazi utadhani chupi la n’kewe” kwa lugha ya kawaida tobo ni sehemu yenyeye uwazi, lakini kwa muktadha wa dikoni mara nydingi huwa na maana ya kuwa makini katika shughuli ya ushonaji nyavu. Mfano mwengine ni pale mtu anapoambiwa kuwa “kwani sie hatuna wake” huwa hawana maana ya kumdhalilisha au kumdharaau ila ni kumtambulisha kuwa ufanisi wa kazi yoyote unategemea zaidi na uchungaji wa muda.

Tukio jengine ni la utani unaofanywa kati ya nahodha na fundi wa chombo.

Nahodha: “fundiii.” (huku akimtikisa mkono)

Fundii: “eeeh!”

Nahodha: “Leo nimekuletea samaki wazuri ukampe shemeji anenepe matakoo.”

Fundi: “lakini utayaona vilevile yale!”

Uhusiano mzuri baina ya watu hujengwa na mapenzi ya kweli na kuthamiana mchango wa kila mmoja kati yao. Mahusiano ya kiutani yaliyopo kati ya fundi wa chombo na nahodha ni dhahiri kuwa huimariswa kwa lengo la kumshajihisha fundi kuwa karibu na nahodha ili anapohitaji matengenezo ya chombo chake asiwe msumbu. Hii humfanya nahodha kila arudipo baharini kuhakikisha anamuwekea kitoweo kizuri ili kumvutia asije akenda kwa nahodha mwengine. Matamshi kama, “nimekuletea samaki wazuri ukampe shemeji anenepe matakoo.” Ni kituko kusikika katika hadhira yenyе silka za kuheshimiana. Lakini, utani huu aufanyao nahodha wakati wa kukabidhi kitoweo hauna maana ya dhihaka wala dharau kuwa fundi hamiliki fedha za kununua kitoweo kizuri bali, kwa maana ya kuutambulisha kuwa thamani yake kwao ni kubwa na kwamba ni mtu muhimu katika maisha ya kazi zao.

Tukio linalofuata kati ya yale yaliyoshuhudiwa na utafiti huu ni lile la kushua vyombo au kuzinduwa chombo, yaani kuweza kukitumia chombo kipyaa kwa shughuli za uvuvi. Hapa hutokea utani wa matendo zaidi ambapo mtu anayetarajiwa kuwa nahodha wa chombo hutoswa majini ili kuonesha umahiri wa nahodha yule pindi pindi anapokuwa baharini. Jambo la ucheshi lililojitokeza ni kuwa katika hali ile nahodha huwa na uwezo wakukimbia kufanya tendo lile la kiutani bali hubakia palepale dikoni ili afukuzwe na akipatikana hubebwa na kwenda kutoswa kwenye chumvi. Hata hivyo, ikiwa atajikomboa huwa hafanyiwi tena. Vilevile, fundi naye hufanyiwa utani unaofanana na huo ili kuonesha umakini wa chombo alichokiunda. Kabla ya kupelekwa baharini kama ilivyotokea kwa nahodha naye hufukuzwa na akipatikana hufungwa kilemba na kibwebwe na kutiwa wanja kisha kupewa nyundo na kuigonga kwa nguvu kuonesha uzima wa chombo hicho.

Tukio jengine la utani ni lile lililotokea ya mnunuzi na mteja sokoni. Linasema:

Muuzaji 1: ‘en’he! Nauza mali yangu wee!’

Muuzaji 2: ‘Haya! Njoo unihurumie mtoto wa mwananamke mwezio we! keroti kutoka Arusha.’

Mteja: ‘haya ba’mkwe kiasi gani?’

Muuzaji: ‘ma’mkwe tia bei mwenyewe unipe utakacho!’

Mteja: ‘Aka! We baba mke kushapata!’

Katika tukio hili utafiti ulishuhudia majibizano ya kiutani kati ya muuzaji na mteja wake. Maongezi kama haya ya kiutani mara nyingi hufanyika kwa mnunuzi na mteja ambae si mara ya kwanza kukutana. Uhusiano kati yao huwa umeshajenga mapenzi na kuhurumiana kulikoimariswa na utani. Kauli ya muuzaji inayosema: “Njoo unihurumie mtoto wa mwanamke mwenzio”. Kuomba huruma kwa mwanamme kwa kigezo cha kuwa naye ni mtoto wa mwanamke ni dhahiri kuwa licha ya kuwa kauli hii ilikuja kiutani, ila mchomo wa hisia za huruma alizojaaliwa mwanamke kutoka kwa muumba, humuongoza kwenye muitiko wa kumsikiliza muuzaji yule japo kwa kuuliza bei tu! Jambo ambalo kwa muuzaji anapokuwa mzigo umemkaa ni faraja seuze kununua.

Ukaribu huu unaotokana na chanzo cha malumbano ya utani hukua siku hadi siku hadi kufikia wawili hao kuwa ndugu. Kwa kuangalia msingi wa nadharia ya utambulisho wa kijamii ambayo utambulisho wa mtu hutumia kigezo cha mila na desturi zilizopo kwa watu wa kundi moja, hapa utani umeonesha jinsi ulivyobeba nafasi ya kuitukuza hadhi ya wanamke kuwa mama wa kila mwanamme.

Tukio lifuatalo lilitokea kati ya nahodha na mwananchi wa kawaida.

Mtani: ‘nahodha eee!’

Nahodha: ‘naam mwamme wasemaje?’

mtani: ‘nahodha nasikia mwaka huu miti yote kuikata kuundu lako jahazi.’

Nahodha: ‘Aaah! Bwana! Wacha mambo yako we!’

Mara nyingine utani huweza kutumika kama jambo la kuonesha istihzai lakini kwa lengo kuchekesha hadhira. Kauli kama hii “nasikia mwaka huu miti yote kuikata” Hapa utani umeonesha mubalagha, maana si kweli kwamba mtu anaweza kuikata miti yote kwa ajili ya kuunda jahazi. Isipokuwa mtani alikusudia kumpa sifa kwa kuamua kutengeneza chombo chake mwenyewe. Pia, katika tukio hili umeonesha utwezaji pale mtani anaposema “kuundu lako jahazi” akimaandisha umeunda jahazi lako. Hapa tunapata kuona kwamba pamoja maongezi haya kuwa na kionjo cha utani bali lugha ya matusi imetumika kuonesha ucheshi.

Tukio jengine ni lile lililosuhudiwa na mtafiti katika bucha ya nyama. Baada ya kuona hali imekua mbaya kibishara muuza nyama alisema:

Muuza nyama 1: ‘jamani! mfupa nnaoooo!’  
Muuza nyama 2: ‘peleka Chumbuni kwa mkeo!’  
Muuza nyama 1: ‘yeye nimempiga mfupa kwanza ndo nikatoka!’

Muktadha wa sokoni hujumuisha uuzaji wa vitoweo mbali mbali kama vile samaki, kuku, nyama na vyengine vingi. Kwa vile biashara hutegemea na siku ilivyopambazukia mfanyabiashara, ni jambo la kawaida sana kwa wauza nyama kubakisha kitoweo chao na kuhifadhi kwenye jokofu kwa ajili ya kuuza siku ya pili. Mara nyingi biashara huwa asubuhi na inapopindukia saa sita huwa ni uuzaji wa kubahatisha. Tukio lisomekalo hapo juu lilijitokeza wakati mfanyabiashara akiwa tayari amekwama katika biashara “jamani mfupa n’naoooooo!”. Kwa kweli, mayowe hayo hupigwa kwa kutumia mbinu ya kiutani ili kutaka msaada pamoja na kujipunguzia machungu ya hasara anayoiyona mbele yake. Aidha, majibu yaliyoitikwa na mwensiwe kuwa apeleke kwa mkewe yaliyonesha kuwa siku ile haikuwa yake na alipaswa kurudi nyumbani. Hata hivyo, ujasiri unaojengwa kupitia

utani humfanya mtu pamoja na majanga tofauti maishani kuwa tayari kupambana hadi ukomo wa maisha yake.

Hali nyingine ya kiutani katika mazingira ya dikoni ilidhihirika kupitia uitaji wa majina ya vyombo. Ni utamaduni wa jamii nyingi kuvipa vyombo majina baada ya kutengenezwa au kununuliwa, hasa vile vitumikavyo kwa biashara. Vyombo hivyo hujumuisha vile vya Baharini na nchi kavu. Wamiliki wa vyombo huandaa majina ya vyombo vyao yasiyo na balagha ndani yake, ila watani hutoa jina jengine lenye maana ya ndani kulingana na ama matukio yaliyopo nchini kwa wakati huo, tabia za wenyе chombo na; simo zilizotawalakwa wakati huo. Kwa mfano, wamiliki wa vyombo huweza kuvipa vyombo vyao majina kama vile ‘HudHud’, ‘Nura’, ‘Nia njema’ na; ‘Kulenga si kufuma.’ Mbali na majina hayo, watani huweza pia kutoa majina ya kiutani. Mifano ya majina hayo ni kama vile ‘Za Mrima tamu’, ‘Ya mkwezi moja’, ‘Mvuli wa Shehe’, ‘Raha ya mwisho’ na; ‘Shangazi mnene.’ Mfano “za mrima tamu” ni jina la utani ambalo asili yake ilitokana na historia ya nahodha wa chombo hicho kuoа wake wa wawili Tanga na mmoja Zanzibar. Huku akiwathamini zaidi wale wa Tanga kuliko wa Zanzibar hapo ndipo watani walipotabiri kuwa za mrima ni tamu zaidi. Kutokana nadharau aliyomfanyia mkewe wa awali watani ndipo walipokipa chombo chake jina hilo. Jina jingine la utani liloitwa chombo ni “ya mkwezi moja” ambalo linatokana na tabia ya mkwezi kupewa nazi moja kila anapokwenda kuangusha nazi lakini katika muktadha wa utani jina hili limejitokeza kimajazi ikifananishwa na tabia ya mtu anayefanya tendo la ndoa kwa mtu asikuwa mkewe kuwa na haraka ya kumaliza kwa hofu ya kukamatwa hivyo mara nyingi nafsi haimpi utulivu wa kuomba aongezwe.

Katika utowaji wa majina ya vyombo hivi utani hujibebesha dhima ya kutambulisha watu wa vyombo vyao ili kuweza kupata umaaarufu. Kwa kutumia nadharia ya Utambulisho wa Kijamii hapa utani unatambulisha tabia za ndani walizonazo kwa kutoa tahadhari kwa wengine kuiga zile zilizo nzuri na kuacha zisizo nzuri kulingana na makubaliano ya makundi yanayounda jamii.

#### **4.4 Athari za Utani wa Dikoni na Sokoni kwa Jamii ya Wazanzibari**

Utafiti ulibaini tija na madhara ya utani utendekao sokoni na dikoni. Hata hivyo, kiasi cha madhara ni kidogo kikilinganishwa na tija zake.

##### **4.4.1 Tija za Utani**

Utafiti ulionesha kuwa utani una tija kwa maisha ya kila siku ya Wazanzibari.

Miongoni mwa tija za utani wa sokoni na dikoni ni :-

###### **4.4.1.1 Kuimarisha Umoja na Mshikamano**

Kihistoria inaeleweka kwamba Wazanzibari ni watu wakarimu wanaoaminiana na kupendana. Mzunguko wa maisha yao ni wa muingiliano mkubwa wa kiudugu. Kwani, mkusanyiko wa watu kumi hadi kumi na tano tu, kwao wao huweza kuibua udugu hasa kwa kuoana. Katika mazingira ya sokoni na dikoni udugu, upendo na mshikamano walionao hukuzwa zaidi na mazungumzo ya kiutani. Kupitia utani wanajamii hawa huweza kushikama na kuonekana kama ni watu wa sehemu moja, pindi wakifika na matukio mbalimbali ndani ya shughuli zao na hata nje ya soko au diko. Mtani huweza kuwa muokozi wako wa awali kwenye tatizo lolote linalokupata katika mazingira ya kazi kama vile sokoni na dikoni. Kwamfano, kuumwa ghafla, litokeapo tukio kama hili pale sokoni au dikoni watu wa awali kukupatia huduma ya kwanza ni marafiki na aghalabu huwa ni watani. Baadhi ya

wakati wanaweza kukuletea utani wakijua nawe unaigiza ila kila muda unavyo songa ukweli wake hudihiri na kutoa msaada wao wa hali na mali. Utaratibu huo huwa ndio huluka ya wahusika wa sokoni au dikoni na hudumu kwani, huwa chachu ya kujenga uhusiano mzuri kati yao. Mtu asiyekuwa na maingiliano mazuri na ucheshi na watu mara nyingi hujikuta akitengwa na kuyaona maisha ni mzigo mzito kwake. Ama kwa watu wenye kuutumia utani kama ni nyenzo ya kujifariji huwa wanapungukiwa na fikra za ugumu wa maisha.

#### **4.4.1.2 Kukuza Uvumilivu na Kuzuia Hasira**

Katika mkusanyiko wa watu wenye mila na tabia tofauti, ni dhahiri kwamba sula la kukosana haliwezi kuepukika. Jambo muhimu la kuzingatia ni kujenga moyo wa uvumilivu na kuzuia hasira. Aghalabu, majibizano ya kiutani hutawaliwa zaidi na ukweli. Ni dhahiri kuwa ukweli unauma ila katika muktadha ya sokoni na dikoni utani hujenga ujasiri na kuvumilia hata kama muhusika ana uchungu moyoni. Mtu anaweza akataniwa na moyoni likamgusa lile aliloambiwa. Hata hivyo, kwa muktadha wa sokoni na dikoni utani unamfanya muhusika avumilie yote atakayo ambiwa na ikibidi kuna utani hawezi kuuvumilia basi anamwita mtani wake faragha, na kumueleza kuwa utani wa aina fulani havutiki nao. Hapo mtu huweza kujengwa uvumilivu kwa mambo mengine yawezayo kumkuta hata kama nje ya mazingira ya sokoni na dikoni. Kwa mfano mzee Mjingi anaeleza kwamba:

Wakati mwengine inaweza kuwa mzigo umekukaa (yaani haujapata mshitiri) basi mtu akutania kwa kuutaka kwa bei ya chini ukahisi kama anakutusi kwa vile hailingani lakini ukavumilia<sup>2</sup>

---

<sup>2</sup> Maelezo haya yamenekuliwa kutoka kwa mzee mjinga tarehe 24/12/2014 wakati akifanya mahojiano na mtafiti.

#### **4.4.1.3 Kujenga Umaarufu**

Katika mandhari ya dikoni na sokoni, utafiti ulionesha kuwa utani unaofanywa na watumiaji wa sokoni na dikoni unasaidia kupata umaarufu. Umaarufu huo ndio humfanya mtu avutie kwa wateja na humfanya mtu awe anauza na kuongeza kipato chake siku hadi siku. Mara nyingi utani wa sokoni na dikoni huanza kwa kupeana majina hivyo, ni rahisi mtu kuelekezwa sehemu yake ya kazi ambapo wateja wanaweza kuvutika na huduma nzuri anazozitoa muhusika kwa uchangamfu wake. Pia, ni faida ndogo ndogo kama za kupata mahitaji ya nyumbani ya kila siku kama vile viungo vya mchuzi, vyakula vya maganda kama, mihogo viazi na mashelisheli kwa wafanyao shughuli zao sokoni. Ama kwa upande wa dikoni, usuhuba walio nao watu uliojengwa na utani huwanufaisha kwa kupata mahitaji yao. Mbali na kitoweo, kwa vile madiko mengi yameingiliwa na uanikaji dagaa, watu wengi kupitia umaarufu wao, huweza kurudi na kuni, chumvi, zilizobakia katika upishi, bila kutozwa fidia yoyote. Mtani anaweza kwenda kwa mtani wake akachukua anacho kitaka bila kutoa malipo yoyote na kesho yake naye akafanyiwa vyivyo hivyo hayo yakawa ndio maisha ya kawaida kwa watu wa sokoni na dikoni. Aidha, umaarufu huo humuwezesha kupata bidhaa za kufanya biashara kwa urahisi na hata asipokuwa na fedha kwa wakati husika. Mtani anaweza kuwa na mtani wake ambaye ni tajiri na ikatokea bidhaa fulani imeadimika kwa wakati ule basi ni rahisi kwa mtani kuweza kupata ile bidhaa kidogo iliyopo kuliko mtu mwingine. Ama kwa upande wa dikoni, watu hutegemea bamvuwa. Yaani, hutokezea baadhi ya wakati kitoweo kikawa adimu hivyo pia kwa mtu na mtani wake nirahisi kupata hicho kitoweo kichache kuliko mwingine na humletea faida kubwa kwa kipindi hicho kwani wateja huwa wengi na wauzaji huwa wachache.

#### **4.4.1.4 Hukosoa na kurekebisha jamii**

Utani kwa uhalisia wake ni dhana inayobeba dhima ya ukweli. Katika ukweli huu utani huweza kumfanya mtu aisute nafsi yake na kufuata mwenendo ulio mzuri. Utani wa sokoni na dikoni, huchukua dhima ya kukosoa na kurekebisha mwenendo wa jamii. Kwa mfano, mtu anaweza kuwa si mlipaji mzuri wakati anapopewa mkopo kiasi cha kuwafanya matajiri washindwe kumhudumia. Baadhi ya wakati, inakuwa ni muhali kumbainishia kuwa deni lako limekuwa kubwa; lakini kuitia malumbano ya kiutani mtu huweza kufahamishwa kuwa hii si tabia njema. Hapa mtani anaweza kumwambia:-

Mtaniwa: ‘Aloo! Hebu nipe mzigo nikatafute kijio (pesa za kutafutia chakula) na watoto.’

Mtani: ‘Nani akupe mzigo, basi hili duka ni la babayo eti uje ukichukuwa mzigo usilipe! Lakini dawa yako iko jikoni.’

Katika malumbano haya ya kiutani, tunaona kwamba ujumbe uliotaka kufikishwa hapa ni kulipa kwa wakati. Mtu huyu endapo atatimiza watu watatu; na wakamjibu majibu kama haya bila kupewa kile anachokihitaji ni dhahiri kuwa atarekebisha tabia yake hiyo ili aweze kukabiliana na maisha. Hapa, utani unamfanya mtu kujirekebisha ili akubaliane na kundi fulani katika jamii kama msingi wa nadharia ya utambulisho wa jamii unaozungumzia ulinganisho katika jamii unavyofafanua.

#### **4.4.1.5 Kuhimiza Ujasiri na Juhudi ya Kufanya kazi**

Utani mara nyingi hubebeshwa dhima ya kuchekesha tu, na kuoneka kwamba ni upuuzi. Katika mandhari ya sokoni na dikoni mbali na kuwa watu hufanya shughuli zao kwa namna ya mtu mmoja mmoja, ziko shughuli ambazo zinahitaji nguvu ya pamoja katika kuzifanya. Kwa kuzingatia hulka ya wanadamu kuwa hawalingani kidesturi, kimila na hata kitabia, utani umechukua nafasi ya kutambulisha tabia tofauti za watu na kuzibadilisha kwa kupenyeza malumbano ya utani ingawa hubeba

na ukweli ndani yake. Katika kuwaelekeza watu kupenda kazi zao utani hutumika kuwahimiza wale wavivu kufanya kazi kwa juhud. Wavuvi shughuli zao mara nydingi hufanywa kwa kikundi na ikitokea mmoja wao kuwa mtegezi basi haiwezekani kumlazimisha kwa nguvu isipokuwa kauli za utani humfanya muhusika ajitambue na kubadilika. Kwa mfano, wakati wa kutweka tanga kuna kamba zinazohitaji ujasiri kuzivuta kwake. Endapo mmoja atafanya utegezi basi hutiwa mori kwa utani kwa kuambiwa “ehe! Vuta kamba iyo, unajiregeza kama mwanamke? Jikaze mtoto wa kiume!” Hapa utani hutoa matokeo ya ujasiri kwa mtaniwa huyo kwa kuzidisha juhud kwenye kazi. Yawezekana mguswaji akajibu kwa utetezi kuonesha sivyo alivyo, bali kwa wakati huo hukaribisha ucheshi tu. Hadhira inayozunguka sehemu ile huwa ina lengo la kuona zao la utani linavyomsukuma mtu kuwajibika kwa kuonesha juhud zaidi ili kuzifanya siku zisogee usoni.

#### **4.4.2 Madhara ya Utani**

Utafiti ulibaini kwamba, utani pamoja na kuwa una tija kama tulivyoziorodhesha hapo awali, ni dhahiri kwamba pia huwa na madhara. Hivyo, nayo tutayaangalia kwa kuyaainisha kama ifuatavyo:-

##### **4.4.2.1 Chanzo cha Ugomvi na Uadui**

Utafiti uligundua kuwa utani kwa upande mwingine huwa ni chanzo cha ugomvi na uadui. Hali hii husababishwa na utani unaopita mpaka, na ule wa kuingiana mwilini. Utafiti uligundua kwamba, mionganoni mwa kauli zinazosababisha mabishano na ugomvi ni utani wa kutajiana wake au wenza. Watafitiwa wengi walionesha kukerwa na tabia hii kiasi ambacho baadhi yao hushindwa uvumilivu na kusababisha uhasama. Pia, utafiti ulionesha jambo jengine ambalo ni kero kwa utani kuwa ni

utani wa kugusana mwili hasa sehemu nyeti kama kiuno, mbavu, na kugusa kidevu kwa mfano wa kutaka kubusu. Kwa mtu anayejiheshimu, hawezi kuwa jasiri kuvumilia matendo haya na ni chachu ya kuzuka kwa sinto fahamu kwa jamii. Watu huweza kufikia hatua mbaya za kuchinjana kwa visu kwa malumbano ambayo awali huonekana kuwa ni ya utani. Akisimulia kisa chake jinsi anavyochukizwa na utani baada kuchinjwa na kisu Bwana Mbaraka maarufu Manyago alisema:-

“Mimi utani kwangu hauna faida, unaiyona kovu hii? Mjomba huyo apo alinichinja kwa jambo la masikhara tu.<sup>3</sup>”

Utafiti ulionesha kuwa mjomba aliyafanya haya baada ya kushindwa kung’amua kuwa alichokuwa akikifanya bwana Manyago kilikuwa ni utani au ni ukweli hata hivyo watu hawa ni marafiki hadi leo.

#### **4.4.2.2 Kuvunjiana Heshima**

Utafiti ulibaini kuwa, heshima, pamoja na kuwa ni kitu cha bure hukosekana kutokana na majibizano, matamshi na matendo ya utani. Hali hii husababishwa na kichocheo cha lugha inayotamalaki sokoni na dikoni kuwa ya matusi. Hivyo, mipaka yake haichagui nani yupo kwa wakati husika. Mtu husema lolote lililopo mbele ya kinywa chake na hutenda lolote lililo katika hisia zake kwa mujibu wa tukio husika lifanyikalo kwa mda ule. Pamoja na kuwa kauli hizo kwa upande mwengine huonekana kuwa lugha iliyokubalika kwa watumiaji wa maeneo husika, haitoi fursa ya kutoziita kauli hizo kuwa ni kauli za kuvunjiana heshima. Kwa mfano, mtu anayekupita na mzigo kuomba kupishwa kwa kusema; “nipe nyuma” au “ehee sokoni hapa” huku akimshika mtu kiuno au “nipe mkeo nilale nae” ni kauli na matendo yanayodunisha hadhi za watu. Hasa wale ambaeo ni watu wa kupita pale sokoni au dikoni. Aidha utumiaji wa mwanamke kwa bezo kama ni kiumbe duni

---

<sup>3</sup> Bw Mbaraka (Manyago) ni mfanya biashara katika soko la Mwanakwerekwe Zanzibar. Mahojiano yake na mtafiti yalifanyika tarehe 25/12/2015 katika soko kuu la Mwanakwerekwe.

kisichoijiweza, husababisha kumvunjia hadhi mwanamke. Kwa mfano, utafiti uligundua kwamba wanaume wengi hushambuliwa kiutani kwa kuambiwa ama, “nipe mkeo”, “nipe dada yako”, “mtoto wa maa”, “una mambo ya kike” na kauli nydingi zinazowiana na hizi. Pia, utani huweza kuwa chachu ya kuvunjiana heshima pale unapofanywa mbele ya watu wanaoheshimiana. Kwa mfano, inaweza kutokea mke au mzee wa mmoja kati ya wahusika kufika katika mazingira ya sokoni au dikoni. Lakini, watani wakaendelea kutaniana wakidhani yule ni mwanamke wa nje, huku wakitoa maneno ya kashfa ambayo hayastahili kusemwa mbele ya mzee au mke. Jambo hili halitomjengea heshima na huweza kusababisha matatizo zaidi hata atakaporejea nyumbani. Kwani huweza kuonekana si mtu muaminifu anapokuwa nje ya familia yake na kuoneka mwenye utii wa woga.

#### **4.4.2.3 Kurudisha Nyuma Shughuli za Kimaendeleo**

Kwa upande wa uchumi, utafiti uligundua kwamba miongoni mwa madhara ya utani ni kurudisha nyuma shughuli za kimaendeleo. Katika hali ya kawaida sehemu za mjumuiko kama sokoni na dikoni, hutegemewa kutoa mchango mkubwa katika pato la taifa. Nguvu kazi iliyopo katika maeneo hayo ni kubwa kuliko ile inayomilikiwa na serekali kiajira. Hivyo basi, mzunguko wa kibiashara huwa ni mkubwa. Kwa vile utani hauepukiki katika maeneo haya ya sokoni na dikoni, baadhi ya wakati huzorotesha shughuli za kimaendeleo. Hii hutokea pale utani unapofanywa wakati kazi imeshamiri. Mtu anaweza kufanya utani kwa kupora vitu hasa vya biashara bila ya ridhaa ya mwenye mali, au kuchukua na kulipia thamani ndogo ya ile bei inayouzwa. Hapa utani husababisha hasara na huweza kuuwa mtaji kwani mtu mmoja huweza kuwa na watani wengi. Vilevile, utani huonekana kuwa kikwazo cha maendeleo pale unapotendwa wakati wahusika wakiwa wameimakinikia kazi na

kuazimia waimalize kwa haraka. Ni dhahiri, inapotokea kufanyiana utani hasa kimatendo inaweza kuchangia kuzorotesha kazi na kurudisha nyuma shughuli za kiuchumi. Kwa mfano, mtu anaweza kuficha vitu muhimu kama ndoo, nyavu, visu, mishipi ambazo ndio zana za kufanya kazi, na kusababisha usumbufo wa makusudi kwa wadau wa shughuli ile. Utani huu unaweza kuchukuwa masaa bila kujali kuwa wakati ni ukuta, na baada ya usumbufo ndio akakurudishia. Hapa utani utakuwa umerudisha nyuma shughuli za maendeleo kwani yale yote yaliyopangwa kutendwa huwa yamedhoofika.

#### **4.4.2.4 Kuimarisha Utamaduni wa Wazanzibari**

Wazanzibari ni watu wanaohifadhi utamaduni wao na kuuendeleza, utani ni moja kati ya amali za urithi kutoka kwa bibi na babu zao. Urithi huo ambao kizazi na kizazi kimekuwa kikiendeleza umekuwa ukitoa athari chanya na hasi kwa utamaduni wa Mzanzibari. Utafiti ulibaini kuwa, athari moja nzuri ya utani kwa utamaduni wa Mzanzibari ni kumtambulisha Mzanzibari kimila na kidesturi kwa kuweka mipaka ya utani kati ya sehemu moja na nyingine, shughuli moja na nyingine na wakati huo huo kuzuia mivutano isiyo ya lazima. Pili ni kurekibisha jamii kwa kuambizana ukweli japo utamuumma moyoni anayeambiwa.

Kiimani, wanadamu wote wanatakiwa kuamrishana mema na kukatazana maovu, lakini mbinu za kukatazana maovu zinatofautiana. Kwa Wazanzibari utani hutumiwa kwa kupongeza na kuasa katika mikradha mbalimbali; ikiwemo ya sokoni na dikoni. Kwa mfano; mtu amekaa muda mrefu hajaowa lakini anafanya uchafu kwa kutembea na wanawake ovyo, watani wake wakamtania “Ewe, babu we! Maziwa yatakuuwa hayo! nunua ng’ombe wako ufaidi nyama na ngozi.” Kauli hizi zinapokuwa zinazisikia masikioni mwake mara kwa mara anaweza akabadilisha

tabia yake na akatafuta mwenza wake. Pia kwa upande mwingine utani unachangia kulinda vazi la heshima la Mzanzibari. Kuvaan nguо za heshima ni moja kati ya mila na desturi za Wazanzibari na endapo mtu atakwenda sokoni na nguо zisizofaa basi watu humtania kwa kusema: “kachukuwe nguо wee!” (huku wakimzomea) au “kajiuze Gofu wewe!” Kauli hizi humfanya mhusika kesho yake asijaribu kwenda sehemu ya mkusanyiko kama ule bila kuvaan nguо za heshima. Kwa maana hiyo utamaduni wa Mzanzibari utakuwa umehifadhiwa. Pamoja na mazuri mengi yaimarishayo tamaduni kupitia utani katika mandhari ya sokoni na dikoni, utafiti umefanikiwa kuibua jambo lenye thamani ambalo ni kubadilishana ladha katika mambo mbali mbali kama vile mapishi, lugha za kilahaja, mavazi, na hata maingiliano ya ndoa. Tukiangalia upande wa mapishi sehemu kama hizi mara nyingi huwa na wanawake wanao uza vyakula ambaо hujilikana kama mama ntilie. Wanawake hawa ni mchanganyiko kutoka sehemu tofauti za Tanzania. Katika kuwafanya watu wakubaliane kitabia, utani hutumika kuwajenga ili wabadilishane fikra katika miktadha tofauti ikiwemo mapishi. Kwa mfano, watu wamrima waweza kuwafunza Wazanzibari kupika vyakula kama, mlenda, makande, ugali, na wao kufunzwa kuandaa keki, vileja, sambusa na vyenginevyo. Kwa dhati utani ni faraja kwa utamaduni wa Mzanzibari

#### **4.4.2.5 Kudunisha Utamaduni wa Mzanzibari**

Kikawaida hakuna jambo lolote lenye kuimarisha lisilokuwa na vichocheo vya kudunisha mwenendo wa asili wa utamaduni wa Mzanzibari. Hivyo pamoja na utani kuwa na faida zinazouwezesha kuimarika, ziko hasara zinazodumaza utamaduni wa Mzanzibari.

Kwanza, ni kuondosha sifa ya ustaarabu wa Wazanzibari, kwani watu wa visiwa hivi tangu kale wamekuwa wakisifika kwa kujiheshimu katika kila nyanja kama vile

lugha, mapishi, na mavazi yao. Utani wa sokoni na dikoni kikawaida umekuwa ukibeba lugha ya matusi, na kwa ugumu wa maisha uliopo visiwani, hata watoto wamekuwa ni wadau katika kufanya kazi ndogo ndogo katika masoko na madiko kama vile kubeba dagaa, kuuza mifuko, maji, na biashara nyinginezo. Hivyo, matusi yanayosikika katika masikio ya watoto hawa yanaweza kuwaathiri hata wanapokuwa mitaani bila ya kujuwa kwamba yale ni kwa mazingira ya sehemu pekee. Mwisho, ni kuporomoka kwa maadili kunakoweza kusababishwa na utani, ambapo utani wa kuashiria matendo ya ngono kama, kumkalia nyuma mwanamke au mwanamme wakati kainama anapara samaki, kutekenyana na hata kujenga mapenzi nje ya ndoa ambapo ni kinyume na mila za Ki-Zanzibari. Hii hutokea zaidi pale baadhi wanapokuwa mbali na familia kwa shughuli za uanikaji dagaa kwa madiko yaliyo nje ya mji. Na hata yale ya karibu ambayo baadhi ya watu wake hawajielewi. Kwa ujumla licha ya kuwa utani ni jadi ya Wazanzibari ila changamoto hizi zimeweza kuwaathiri utamaduni halisi wa Mzanzibari.

#### **4.5 Hitimisho**

Sura hii imejadili matokeo ya uchambuzi wa data zilizokusanywa kutoka uwandani na maktabani. Mjadala huu uligawanywa katika sehemu kuu tatu. Mambo ya msingi yaliyojadiliwa katika sehemu hizo ni: sababu zinazopelekea kuzuka kwa utani wa sokoni na dikoni kwa jamii ya Wazanzibari, utendaji wa utani wa sokoni na dikoni unaohusisha utani wa maneno na wa matendo, sampuli za matukio ya utani wa sokoni na dikoni na hatimaye athari za utani kwa jamii ya Wazanzibari zikioneshaa uimarishaji na udunishaji wa utamaduni. Katika sura inayofuta utafiti unaelezea muhtasari, hitimisho, maoni na mapendekezo juu ya tafiti zijazo.

## **SURA YA TANO**

### **MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

#### **5.1 Utangulizi**

Sura hii inawasilisha muhtasari na hitimisho la tasnifu hii. Kadhalika, sehemu hii imetoa maoni kadhaa yaliyopatikana kutokana na utafiti huu. Aidha, sura hii imeelezea ufaafu wa nadharia na kutoa mapendekezo kwa tafiti zijazo.

#### **5.2 Muhtasari wa Tasnifu**

Utafiti huu ulilingalia nafasi ya utani wa sokoni na dikoni kwa jamii ya Wazanzibari ambayo ililifafanua sababu, muundo na athari zake kwa jamii ya Wazanzibari. Tasnifu imegawika katika sura tano, ambapo kila sura imeeleza mawazo yake makuu kwa muhtasari.

Sura ya Kwanza imetoa muelekeo wa tasnifu hii kwa kuanza na maana ya istilahi zilizotumika katika utafiti huu, historia ya utani, pamoja na aina za utani. Pia, utafiti ulitoa taswira juu ya usuli wa mada, malengo ya utafiti, likiwemo lengo kuu na malengo mahsus. Vilevile, imeonesha maswali ya utafiti umuhimu wa utafiti, tamko la utafiti na kumalizia kwa nadharia iliyotumika katika utafiti huu.

Sura ya Pili imefafanua maandiko yaendayo sambamba na utafiti huu. Maandiko mbalimbali yahusuyo dhana ya utani na jamii ya Wazanzibari kama vile vitabu, makala, majarida, tafiti tangulizi na tovuti mbalimbali zilisaidia katika kuibua mapengo ya utafiti huu ambayo yalitoa mwanya wa kuweza kuangalia utani kwa upande dikoni na sokoni.

Sura ya Tatu imeeleza mbinu na vifaa viliviyotumika katika utafiti huu. Sura hii inabainisha muongozo kamili wa utafiti ulivyokuwa, aina ya kundi lililohitajika kwa

ajili ya kutoa majawabu juu ya maswali ya utafiti pamoja namna data zilivyokusanywa na kuchambuliwa kwa kuongozwa na nadharia iliyochaguliwa ambayo ni nadharia ya Utambulisho wa Kijamii katika utafiti huu.

Sura ya Nne imeonesha namna data zilivyowasilishwa na kutafsiriwa. Aidha, malengo na maswali ya utafiti ambayo yalijibika na kugawika katika sehemu tatu kuu. Kwanza kutoa sababu za kuzuka utani kwa jamii ya Wazanzibari. Pili ni muundo wa utani wa sokoni na dikoni na hatimaye athari za utani kwa jamii ya Wazanzibari.

Sura ya Tano inahusu hitimisho la utafiti huu kwa ujumla wake ikijengwa na muhtasari wa kazi, matokeo ya utafiti, utoshelevu wa nadharia, pamoja na mapendekezo juu ya tafiti zijazo.

### **5.3 Utoshelevu wa Nadharia Iliyotumika**

Nadharia ya Utambulisho wa Kijamii ndio iliyotumika katika kukusanya data na uchambuzi wake. Nadharia hii imebeba mambo makuu matatu ambayo ni: utambulisho katika jamii, ulinganishi katika jamii na matabaka katika jamii. Msingi wa mwanzo ni utambulisho katika jamii. Hapa ni pale mwanadamu anapojitambulisha yumo katika kundi gani kwa kupitia mila na desturi zilizopo ambazo amezipata kutoka katika jamii anayoishi nayo. Msingi wa pili ni ule wa ulinganishi katika jamii, ambapo mtu anaiga kutokana na kuvutiwa na mtu au kundi la watu kwa kufuata mila na desturi zilizopo. Na mwisho ni msingi wa matabaka na mgawanyiko katika jamii ambapo njia hii huamua kundi la mtu linalomfanya aweze kushiriki jambo lolote bila ya mzozo. Misingi ya nadharia hii imetusaidia sana katika kuibua nafasi ya utani kwa jamii ya Wazanzibari. Nadharia hii imetusaidia kubaini

kuwa, utani unaofanyika katika masoko na madiko umekua ukiwatambulisha watu katika miktadha tofauti kama vile ya kazi zao, hadhi zao, asili yao, mila na desturi zao. Utani umekua kitambulisho cha kuweza kutofautisha matabaka yaliyomo katika mandhari ya sokoni nadikoni kwa mujibu wa shughuli mahsus wazifanyazo kila uchao. Hivyo, nadharia hii imefaa katika kutafiti nafasi ya utani wa sokoni na dikoni kwa jamii ya Wazanzibari.

#### **5.4 Mambo Mapya Yanayoibuliwa na Tasnifu Hii**

Mambo mapya yaliyomo katika tasnifu hii ni haya yafuatayo:

Kwanza, utafiti umebaini kuwa, kuna tofauti kubwa kati ya sababu zinazopelekea kuzuka utani kwa jamii ya Wazanzibari katika muktadha wa sokoni na dikoni, ukilinganisha na utani kama wa harusini, msibani na ule wa makabila. Mbali na sababu kuu ya kujenga udugu na ushirikiano, pia kuna sababu nyengine ambazo zinaupa utani wa sokoni na dikoni upekee wa aina yake. Sababu za ziada ni kama zile za kujipatia umaarufu ambao humfanya muhusika kuweza kusambaza huduma zake za kibashara kiurahisi na kumpatia mahitaji yake muhimu ya kila siku. Hizi ni zinajitofautisha na sababu zilizopelekea utani kwa makabila ambazo huwa ni njaa na vita na zile za harusini ambazo mara nyingi huwa ni uhusiano wa kiukoo.

Pili, muundo wa utani wa sokoni na dikoni. Utafiti huu umeibani kuwa utani wa sokoni na dikoni unajikita zaidi kimaneno kuliko kimatendo kama vile utani wa harusini au msibani. Maneno mengi yatumiwayo kiutani kwa watu wa sokoni na dikoni ni ya matusi na ubeuzi wa hali ya juu, ambayo ni aibu kutumika katika miktadha ya kawaida. Kwa upande wa utani wa matendo hupungua zaidi kwa sababu, sehemu za sokoni na dikoni ni sehemu ambazo ziko maalumu kwa kufanya kazi hivyo utani wa matendo ukishitadi zaidi huweza kuzorotesha shughuli za kazi

ambazo ndio msingi wa maendeleo. Hata hivyo, utani wa matendo hufanywa kwa kiasi kidogo ingawa unaonekana kuchukiwa na watu wengi hasa wale wanaojali kazi zao.

Tatu, utafiti huu uligundua kuwa utani wa sokoni na dikoni hauzingatii uhusiano wa kiudugu wala kiukoo, bali huwa kama urafiki tu, ambao baadaye huzalisha udugu. Katika mahusino ya utani wa sokoni na dikoni watu hujenga upendo na kuaminiana kiasi cha kuthubutu kujenga udugu kwa kuozeshana ili kuendeleza mahusiano walionayo. Hata hivyo; utafiti umebaini kuwa mahusiano hayo ya kiutani yanapojengeka zaidi kwa watu wawili wenye jinsia tofauti, huweza kuleta fitina na kupelekea uhusiano wa kimapenzi nje ya ndoa, ambapo ni kinyume cha utamaduni wa Mzanzibari na utamaduni wa Kiislamu kwa ujumla.

Mwisho, imezoeleka katika masikio ya watu kuwa utani una lengo la kufurahisha na kunogesha jambo. Kwa mfano, katika shughuli ya harusi hunogesha na kuifanya shughuli ivutie na ichangamke. Hata kwenye msiba utani una lengo la kuondoa simanzi na machungu ya kuondokewa, lakini kwa muktadha wa sokoni; utani una nafasi ya kuivuta hadhira ya wateja na kutambulisha shughuli zao wazifanyazo aidha iwe sokoni au dikoni.

### **5.5 Maoni ya Mtafiti juu ya Utafiti Huu**

Utafiti huu napendekeza maoni yafuatayo kushughulikiwa ili kuisaidia jamii:- Mosi, kutokana na umuhimu wa utani kwa jamii ya Wazanzibari inapendekezwa kuwa Wizara ya habari utamaduni na michezo itoe taaluma kwa jamii juu ya umuhimu wa utani, na kuiepusha jamii kuziona tamaduni za kimagharibi kuwa ni bora kuliko mila zetu.

Pili, kwa vile utani wa sokoni na dikoni unatawaliwa zaidi na kauli za kejeli na matusi mtafiti anapendekeza wahusika wajichunge kuzitumia lugha zile wanapokuwa majumbani ili kuepusha wigo kwa watoto wadogo wa kuzitumia lugha hizo kama lugha ya kawaida.

Tatu, mtafiti anapendekeza kesi zitokanzo na utani zisichukuliwe ni za kiutani tu, bali zipelekwe katika vyombo vya sheria na kupatiwa hukumu inayofaa kwani zikiachiwa tu hazitopungua bali zitaongezeka na kukitia dosari kipengele hiki cha utani.

### **5.6 Mapendekezo wa Tafiti Zijazo**

Kukamilika kwa tasnifu hii haimaanishi ya kwamba ni mwiko kwa wengine kutafiti katika kipengele hiki cha fasihi. Hii ni kwa sababu utafiti huu ulikuwa na malengo na mipaka yake. Hivyo, bado kuna maeneo kadhaa ambayo yanatakiwa yafanyiwe kazi na watafiti wengine. Maeneo yanayopendekezwa ni:-

- a. Mtafiti anapendekeza utafiti mwingine ufanywe juu ya dhamira za majina ya utani wanayopewa watu katika jamii. mandhari ya sokoni yanahuisha amali hii ya utani na hunogeshwa utani huo kwa wahusika wa utani kupeana majina ya utani, ambayo kwa matamshi ya majina hayo hayapangwi isipokuwa kwa mnasaba maalum.
- b. Uwanja mwengine ambao unaweza kumakinikiwa na watafiti wajao ni kulinganisha na kulinganua kati ya utani wa sokoni na ule unaofanwyka katika sehemu za kazi, dhima na athari zake kwa jamii.
- c. Yafanyiwe utafiti malumbano ya kiutani kifani na kimaudhui, ili kugundua ujumbe unaopatikana katika kauli zitolewazo na watani.

## **MAREJELEO**

- Adowole, J.M (1984), “Agreement as a cohesive devices in Kiswahili, M.A dissertation, university of dare s salaam: Tanzania (haijachapshwa)
- Bakiza (2008), *Utamaduni wa Mzanzibari*, Quark Express Printing Services, Zanzibar.
- Bakiza, (2010), *Kamusi la Kiswahili Fasaha*, Oxford University Press. Nairobi, Kenya.
- Benne, J. (1974), *The Masai, Katika Utani Relationship in Tanzania*. Vol.III, Dar es Salaam University Press
- Bukanya na wenzake. (2005), *Oral Literature as Senior Course*, Longhorn Publisher (K) Ltd, Nairobi Kenya.
- Chogero, B. (1971), *The Socio-Economic Implications of Utani in Jita Society*. Dar es Salaam University Press.
- Devie C. (2005), *Jokes and Groups*, The Institute of Cultural Research, Antony Rowe Ltd, London.
- Gbotokuma, Z. (1998), *Cultural Identity and Underdevelopment in Sub Saharan Africa*, Voice from Africa uk.17-19
- Ghasani, M.K (2006), “Kheri ya Ruhani Kuliko Subiani”, Zanzibar Daima Iliyosomwa Tarehe 16/11/2014 kutoka.  
[www.zanzibardaimawordpress.com](http://www.zanzibardaimawordpress.com).
- Gora, H. (1999), *Utenzi wa Visa vya Nabii Suleiman bin Daud*, Al-Khayria Limited, Zanzibar.
- Haji, M. (2006), *Vipera vya Fasihi Simulizi*, Central Publishing Services Tanzania, Zanzibar
- Iddi, Z. (2011), “Dhima ya Utani kwa Wazanzibari”, Ripoti ya Utafiti kwa Ajili ya Shahada ya Awali Chuo Kikuu cha Taifa SUZA, (Haijachapishwa).
- Juma, K. (2008), *Kiswahili cha Asili cha Wanawake wa Visiwani Zanzibar*, Quark Express Printing Services, Zanzibar.

Kahigi, K.K na Mulokozi, M (1979), *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*, Tanzania Publishing House, Dar es Salaam.

Kombo, D. na Tromp, D. (2006), *Proposal and Thesis Writing, An Introduction*, Paulines Publications Africa.

Kothari, C. (2003), *Research Methodology and Techniques*, New International, (P) Ltd New Delhi.

Kyando, A.S.J. (1973), *The Kinga*, URT, Vol.II, Dar es Salaam University Press.

Makame, C. (1973), *The Bondei Utani Relationship*, Vol.1, pp 40, Dar es Salaam.

Mboga, J.J. (1975), *Yao Marriage, Clan Utani, Land Ownership and Ancestor Propitiation: A Study of Chiwata Village Customs*. URT, Vol.VI, Dar es Salaam University Press.

Mfikiriwa, S. (1970), *The Doe*, Utani Relationship Vol.1, pp.55, Dar es Salaam.

Mgakanzila M. (2010), *The Basukuma Jokes*, Aera Kiswahili Researched Products, Dar es Salaam

Mkubwa, C. (2012), “Dhima za Utani Katika Mazishi na Matanga ya Wapemba na Athari Zake kwa Jamii” Ripoti Ndogo ya Utafiti Kwa Masharti ya Kutunukiwa Shahada ya Sanaa (Ualimu) Katika Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii. Chuo Kikuu Cha Waislamu Morogoro (Haijachapishwa)

Mrikaria, S E. (2010), Kejeli na Fasihi ya Kiswahili Tanzania, *Swahili forum17*

Msokile, M (1992), *Misingi ya Hadithi Fupi*, Dar es Salaam University Press, Da es Salaam.

Msuya, S. (1978), *Yatokanayo na Fasihi Simulizi*, Tanzania Publishing House, Dar es Salaam.

Mulokozi M.M. (1989), Tanzu za Fasihi Simulizi, Mulika Namba 21, TUKI. Dar es Salaam.

Mulokozi M.M. (1996), *Utangulizi Wa Fasihi ya Kiswahili*, Chuo Kikuu Huria Cha Dar es Salaam, Tanzania.

Mzandi, M. (2011), “Nafasi ya Utani Msibani na Harusini kwa Kabilia la Wadigo”. Ripoti ya Utafiti kwa Ajili ya Shahada Umahiri Chuo Kikuu cha Dodoma, (Haijachapishwa).

Ntarangwi, M (2004), *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*, Austina College, RockIsland, IL61201

Nunan, D. (1972), *Research Methodology in Languge Learning*, Combridge University Press : Combridge.

Ogacho, O. (1974), *Grandparent-Grand Children Utani*, URT, Vol.III, Dar es Salaam University Press.

Ogech, N na wenzake. (2008), *Nadharia katika Taaluma za Kiswahili na Lugha za Kiafrika*, Moi University Press.

Ponera, A.S. (2010) “Athari za Ufutuhi Katika Nathari za Shaaban Robert: Maana, Matumizi na Athari Zake kwa Wasomaji”. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dodoma. (Haijachapishwa)

Ponera, A.S. (2014), “Ufutuhi katika nathari ya Kiswahili Ulinganisho wa Nathari za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi”, Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu katika Fasihi ya Kiswahili Chuo Kikuu Dodoma.

Ritti, A. (1970), Utani Relationship, The Arusha in Vol. 1, 2 pp5-7

Sengo, T.S. na Lucas (1975), *Utani wa Jamii ya Wakwere*, Nairobi Foundation Book Limited, Nairobi.

Senkoro, F EM K (1982), *Fasihi*, Press Capability Center, Dar es Salaam.

TUKI (2004), *Kamus ya Kiswahili Sanifu*, Oxford University Press, Nairobi

Walliman, N. (2011), *Research Method the Basic*, Routledge Taylor and Francics Group, London and New York.

Yahya-Othman, S na wenzake (haina tarehe), “Structure and Function of Jokes in Tanzania, Ripoti ya Utafiti Mdogo”, Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

Zeid O. (2011),”Athari za Lugha ya Utani Katika Jamii ya Wapemba,” Ripoti ya Utafiti kwa Ajili ya Shahada Umahiri Chuo Kikuu cha Kiislam Uganda, (Haijachapishwa).

## VIAMBATISHO

### **A: Mwongozo wa Usaili kwa Wataalamu wa Fasihi**

1. Unafahamu nini kuhusu utani katika mazingira ya hapa sokoni/dikoni?
2. Ni zipi shughuli zako za kila siku ufikapo sokoni au dikoni?
3. Unahisi kwa nini watu hutani ana kwenye mjumuiko wa sokoni au dikoni
4. Je, wewe unafurahishwa na utani? Ikiwa ndiyo/hapana kwa nini?
5. Je, utani wa sokoni au dikoni unatumia njia gani zaidi kati ya maneno au matendo?
6. Je, unapata faida gani kiuchumi, kiutmaduni au kijamii unapotaniwa au kutania?
7. Je, unahisi ipo haja ya kuendeleza utani kwa wanajamii ya Kizanzibari? Ikiwa ndiyo/hapana kwa nini?
8. Je, matendo ya utani wa sokoni /dikoni yana uhusiano na utamaduni wa Wazanzibari? Ikiwa ndio/hapana kwa vipi?

### **B: Dodoso kwa Wataalamu wa Fasihi**

1. Unafahamu nini kuhusu dhana ya utani?

.....

.....

2. Taja sababu mbili tu za kuzuka kwa utani kwa jamii ya wazanzibari

i) .....

ii) .....

3. Taja maeneo muhimu ambapo utani huwa unatokea mara kwa mara kwa Wazanzibari

.....

.....

4. Je utani wa sokoni na dikoni hufanyika kwa maneno au kimatendo zaidi?

.....

.....

5. Je utani una uhusiano na utamaduni wa Zanzibar? Ndiyo [ ] Hapana [ ]  
Kama jibu ni ndiyo, eleza kwavipi .....

6. Je kuna athari zozote za kiuchumi, kijamii au kiutamaduni kwa mtaniwa kwa watumiaji wa soko au diko? Ndiyo [ ] Hapana [ ]

Zitaje? .....

7. Je kuna haja ya kuendelea na amali hii ya utani kwa jamii ya Kizanzibari? Ndiyo [ ] Hapana [ ]

a) Toa sababu

.....  
.....  
.....

**C: Picha Mbalimbali Zinazohusiana na Utafiti**



**Picha namba 1: Mtafiti wa pili kulia akiwafanyia usaili wapishi wa dagaa katika diko la Maruhubi Mjini Zanzibar tarehe 22/12/2014. (utafiti 2015) )**



**Picha namba 2: Mtafiti akimuhoji mfanya biashara katika soko la Mwanakwerekwe Zanzibar tarehe 24 /12 /2014 (Utafiti 2015)**



**Picha namba 3: Mtafiti akiwa katika mnada wa nazi katika soko la mboga mboga Mombasa Zanzibar tarehe 24/12/2014 (chanzo mtafiti)**



**Picha namba 4: Wavuvi wakitaniana utani kimatendo katika diko la maruhubi  
tarehe 22/12/2014 (Utafiti, 2015)**